**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais |
| 2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani. |
| 3.Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais |
| 4.Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu |
| 5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa |
| 6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa |
| 7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 8.Mhe. Hamad Masoud Hamad | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole. |
| 9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa |
| 10.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa |

| | |
|---|---|
| 11.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa |
| 12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni |
| 13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge. |
| 14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki |
| 15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni |
| 16.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando |
| 17.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi |
| 18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe |
| 19. Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni |
| 20.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 21.Mhe.Othman Masoud Othman | Mwanasheria Mkuu |

| | |
|---|---|
| 22.Mhe. Issa Haji Ussi | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka |
| 23.Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake |
| 24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya | Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais |
| 25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake |
| 26.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi |
| 27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni |
| 28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 30.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 31.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini |
| 32.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa |
| 33. Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 35. Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 36.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 37.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 38.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 40.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 42.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 43.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 44.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 47.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Jimbo la Kikwajuni |
| 49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa | Jimbo la Mkwajuni |
| 51.Mhe. Mgeni Hassan Juma | Nafasi za Wanawake |
| 52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 53.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad | Jimbo la Chambani |
| 55.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Jimbo la Mpendae |
| 56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Nafasi za Wanawake |
| 57.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 58. Mhe. Mussa Khamis Silima | Jimbo la Uzini |
| 59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 61.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |
| 62.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 63.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Rashid Seif Suleiman | Jimbo la Ziwani |
| 65.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 66.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 67.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 68.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 69.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 70.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 71.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni |
| 72.Mhe. Salum Amour Mtondoo | Jimbo la Bububu |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan | Jimbo la Dole |
| 76.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim** — **Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

**Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 29 Julai, 2011**

*(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)*

**Dua**

*Mhe. Spika,(Mhe. Pandu Ameir Kificho) Alisoma Dua.*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha mezani hotuba ya kuwasilisha mswada wa sheria wa kuidhinisha makisio na matumizi ya serikali kwa mwaka 2011/2012 naomba kuwasilisha.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya kuwasilisha mswada wa sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, kazi zake na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Vile vile naomba kuwasilisha mezani hotuba ya kuwasilisha mswada wa sheria ya kuweka masharti ya utawala udhibiti na uendeshaji wa viwanja vya ndege Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman, Makamo Mwenyekiti: (Kny:Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi):** Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti, wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, kuhusu mswada wa sheria ya kuanzisha mamlaka ya viwanja vya ndege Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo, pamoja na mswada wa sheria ya kuweka masharti ya utawala, udhibiti na uendeshaji wa viwanja vya ndege Zanzibar pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

## MASWALI NA MAJIBU

### Nam 219

### Bandari na Uchumi wa Taifa

**Mhe. Hija Hassan Hija** - Aliuliza:-

Bandari ni eneo na chanzo kizuri cha kuongeza na kukuza mapato na uchumi wa Taifa hasa katika nchi za Visiwa. Kwa kuzingatia jambo hilo nchi nyingi duniani zimekuwa zikiimarisha bandari zao. Mfano mzuri ni ule uwamuzi wa SMT kujenga bandari ya kisasa huko Bagamoyo itakayokuwa na uwezo wa kuchukua makontena 14,000.

(a) Wakati wenzetu wa SMT wana mpango wa kujenga Bandari hiyo ya kisasa, juhudi za ujenzi wa bandari ya Mpigaduri na Mkumbuu zimefikia wapi .

(b) Je, Bandari yetu ya Malindi inauwezo wa kuchukuwa makontena mangapi kwa wakati mmoja.

(c) Zanzibar kama kisiwa itaathirika vipi na ujenzi huo wa Bandari ya Bagamoyo.

(d) Bandari zetu Zanzibar huchangia kiasi gani kwa pato la Taifa kwa mwaka mmoja.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 219 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Napenda kumjuilisha Mhe. Mwakilishi kuwa Serikali kupitia Wizara yangu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, inaendelea na juhudi za uratibu wa Mradi wa Ujenzi wa Bandari Mpya hapo Mpiga Duri, ambapo tayari tumesaini Makubaliano ya Awali (*MOU*) na Kampuni ya Ujenzi ya *China Road and Bridge Corporation (CRBC).*

Mhe. Spika, makubaliano hayo yanahusisha uanzishaji wa mashirikiano baina ya pande mbili hizo katika kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Bandari Mpya ya Mpiga Duri. Ndani ya makubaliano hayo Kampuni ya *CRBC* itakamilisha ripoti ya Upembuzi Yakinifu (*Feasibility Study*) pamoja na utafutaji mtaji, uchoraji na ujenzi katika mfumo wa "*Engineering, Procurement and Construction*" (*EPC*). Hivi karibuni Wizara yangu iliwapeleka Wataalamu wake wawili nchini China ili kushirikiana na Wataalamu wa Kampuni ya *CRBC* kuharakisha ukamilishaji wa ripoti ya Upembuzi Yakinifu ambapo inategemewa itakuwa tayari muda mfupi ujao.

Mhe. Spika, Baada ya kukamilisha ripoti hiyo Serikali itawasilisha maombi ya Mkopo (*loan*) katika Benki ya *Exim* ya nchini China kupitia Wizara ya Fedha ya Muungano (*SMT*) kwa mujibu wa utaratibu wa Benki ya *Exim*.

b. Mhe. Spika, Bandari ya Malindi ina uwezo wa kuchukua makontena karibu 2000 kwa wakati mmoja, makontena hayo yakiwa yanapangwa matatu kwenda juu.

c. Mhe. Spika, Zanzibar haitoathirika chochote na ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo hasa kwa sababu wakati huo Bandari hiyo ya Bagamoyo itakuwa imejengwa, Zanzibar nayo inategemea kuwa bandari mpya ya Mpigaduri itakuwa tayari imeshajengwa na itaweza kushindana na bandari za ukanda wa Afrika Mashariki.

d. Mhe. Spika, Shirika la Bandari linachangia kwa sehemu kubwa katika pato la taifa kwa kupitia taasisi za fedha haza TRA na ZRB katika ukusanyaji wa mapato kwa kupitia malipo ya forodha pamoja na mambo mengine.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a),(b), na (c) kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kama tunavyojua bandari ni suala la Muungano, ingawa haliendeshwi Kimuungano kati ya Tanganyika na Zanzibar, kila upande unaendesha shughuli zake. Shughuli hizi za bandari zinategemea sana kuwepo kwa minara ya mawasiliano. Minara hii huchangia mapato sana.

(a) Mhe. Spika, naomba kujua Zanzibar inapata mapato kiasi gani kutokana na minara hii ya mawasiliano kwa ajili ya kuwawezesha wenye meli na taasisi nyengine kuingia kwenye minara yetu Zanzibar.

(b) Mhe. Spika, nimemtaka Mhe. Waziri aniambie mchango wa bandari kwa pato la taifa, naomba kujua bandari yetu ya Zanzibar inamechangia kiasi gani kwa pato la taifa.

(c) Mhe. Spika, naomba kujua mwaka jana na mwaka juzi wizara yake ilizungumzia ujenzi wa Bandari ya Mkumbuo pamoja na matengenezo ya kisasa kwenye Mnara wa Kigomasha kule Pemba. Naomba kujua hatua hii imefikia wapi, wakati bajeti ya mwaka huu haijasema lolote.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, ni kweli Shirika la Bandari limekuwa na utaratibu wa kugawana mapato na Shirika la Bandari la Dar es Salaam mapato yatokanayo na minara.

(a) Mhe. Spika, katika makubaliano yetu Shirika la Bandari Zanzibar na Shirika la Bandari la Dar es Salaam tunagawana kwa mfumo wa Zanzibar kupata 49 na Bara wanapata 51. Mapato ya minara yanatokana na huduma za meli. Wanaopokea meli nyingi ni wenzetu wa Tanzania Bara, lakini wamekubali mapato yale tutagawana kwa *quarter* tatu kwa mwaka na kila *quarter* hakuna tunazokosa chini ya milioni 150.

(b) Mchango wa Bandari katika pato la taifa tumeeleza kwamba bandari inahusishwa katika mchakato wa eneo na usafiri katika pato la taifa. Tumeeleza kwamba ushuru wa forodha wanaojua takwimu sahihi ni wenzetu wa Wizara ya Fedha, lakini sisi kama bandari tunapata fedha takriban bilioni 8, mapato yaliyopatikana mwaka jana.

(c) Mhe. Spika, ni kweli kwamba tulieleza kuwa Bandari ya Mkumbuu tuna mpango wa kutaka kuiendeleza. Ni kweli kuna wenzetu tunaendelea na mchakato Kampuni ya *Ocean Fruit* wameshaleta maombi ya kutaka kwenda kuona eneo hilo ili kuendelea na usanifu na mambo mengine. Lakini kwa upande wa Mnara wa Kigomasha. Mhe. Spika, napenda kulithibitishia Baraza lako hili tukufu mnara huu umetengenezwa, uko vizuri na yeyote anayetaka kwenda kuuona, tuko tayari kumpeleka kwenda kuhakikisha hilo.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Naibu Waziri ametuambia kwamba Bandari ya Malindi ina uwezo wa kuchukua kontena 2,000.

(a) Je, huoni kuwa ile bandari utaimaliza hivi sasa kutokana na matatizo iliyokuwa nayo imeshaanza kubonyea.

(b) Kuna mpango gani wa kuanzisha bandari Nungwi ili kuweza kuwapunguzia usumbufu wananchi wanaokwenda Pemba, ukitizama kutoka Nungwi mpaka Pemaba ni masafa mafupi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, pamoja na maelezo ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub na sababu nyengine, ndio maana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikafikiria wazo la kujenga bandari mpya ya Mpigaduri.

(a) Matokeo yetu ni kwamba tutakapoweza kujikomboa na kujenga bandari yetu mpya ya Mpigaduri, basi malalamiko haya na hisia nyengine zitakuwa zimeondoka.

(b) Mhe. Spika, kwa muda huu tunaendelea kuzungumza na wenzetu waliloonesha nia ya kutaka kufanya upembuzi yakinifu na mambo mengine kwa kuangalia eneo la Mkokotoni, hasa eneo la Fukuchani ili ikiwezekana tukiweza kupata nguvu na wakati ukifika kujenga bandari katika eneo lile.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Zanzibar tuna bandari moja tu ambayo ina uwezo wa kuchukua makontena na meli kubwa za mizigo na kuweka pale na kwa kuwa Zanzibar sasa hivi tuna mpango wa kuwekeza, aidha viwanda na kwa ajili ya kukuza uchumi weu zaidi. Kwa kuwa eneo la Mkumbuu ni zuri na lina kina kikubwa cha maji kinachoweza kusaidia bandari yetu iliopo Zanzibar na kwa kuwa Mhe. Waziri amesema kuna wafadhili au wajenzi wamekuja kutaka kuona Mkumbuu kwa ajili ya kusaidia.

Je, ni lini hasa serikali itaona kwa kupitia wizara yake hii kuwapeleka hao jamaa Mkumbuu kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa bandari nyengine na kusaidia kufika meli za makontena.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii, naomba nimjibu Mhe. Subeit Khamis Faki jibu la ziada. Mhe. Spika, jibu la Mhe. Naibu Waziri lilitosha, lakini mimi namuongezea tu, kwa sababu Naibu Waziri alijibu kuhusu Mkumbuu.

Mhe. Spika, katika *Zanzibar Transport Master* Plan tuna bandari maalum ambazo zimepewa kipaumbele. Moja ni Mpigaduri ambayo maelezo yake yameelezwa vizuri, hiyo ni bandari kubwa na nyengine kubwa ni Bandari Mkumbuu. Lakini katika mambo haya kuna kipaumbele, huwezi kuchukua mambo yote ukajitwika. Kwa hivyo, mtazamo wetu mkubwa sasa hivi ni Bandari ya Mpigaduri, lakini na hii ya Mkumbuu haijasahauliwa, tumewaalika makampuni mengi moja ikiwa ni hii Kampuni ya Ocean Fruit ambao kwa mawasiliano ya karibu ni kwamba wakati wowote watatuambia ni lini watafika Zanzibar kwa ajili ya kukaa kitako tukawaonesha maeneo halafu tukakubaliana watafanya lipi na lipi. Hilo ni moja.

Vile vile kuna kampuni nyengine ya MKM, hiyo ni Kampuni ya Uholanzi na wameonesha hamu ya huko huko Mpigaduri, kwa sababu wana historia ya Mpigaduri miaka labda 30 nyuma. Kwa hivyo, bandari zote mbili ambazo ni kipaumbele na ambazo zitakuwa ni bandari kubwa kwa Zanzibar na zitafufua uchumi kwa kiasi kikubwa watu wasichotegemea. Tunazishughulikia kwa kiasi hicho na kwa hivyo wakati wowote watakapokuja tukakubaliana ndipo tutakapowapeleka kule kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na hatimaye kufanya shughuli nyengine zinazoendelea.

Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe waelewe kwamba juzi tumepokea *feasibility study* iliyofanywa na *CBRC*. Leo ni siku ya tatu tangu kupokea, ni kwamba hii imemalizika na *copy* hizi tunapeleka Wizara ya Fedha na wizara nyengine, ili wachangie tupate maoni tuyapeleke ili wao wafanye *final report* ya hiyo *study*, haitochukua zaidi ya mwezi mmoja. Baada ya *study* hiyo, gharama za kufanya mambo mengine *detail design and tender document* zitafuata. Baada ya hapo ndipo *exactly* utajua ni kiasi gani kitagharimu ujenzi wa barabara yetu.

Lakini Mhe. Spika, katika hii *draft report* ambayo tumeiwasilisha juzi, basi ujenzi huu unakisiwa kugharimu katika *Phase* zote tatu. Maana yake ni *phase I, phase II* na *phase III*, ambapo phase zote tatu zitakuwa na eneo la hekta 320. zitagharimu dola za Kimarekani milioni 682. Lakini *exactly cost* ya *phase* zote tatu itajulikana baada ya matayarisho ya *tender document.* Kwa hivyo, hii ni taarifa kwa wajumbe na nilisema nilifafanuwe vizuri ili ionekana kwamba hatua zinachukuliwa na ni hatua madhubuti. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

**Nam. 232**

**Upungufu wa Maji Mjini Magharibi**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza:-

Ni ukweli usiopingika kwamba huduma ya maji safi na salama katika baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi bado ni tatizo. Hata hivyo, Serikali baadhi ya wakati huwa inajipiga kifua kuwasaidia wananchi. Hili ni jambo zuri ingawa Serikali haina gari lake la kubebea maji .

(a) Serikali haioni kwamba kukodi magari ya maji kunapoteza fedha nyingi za umma.
(b) Je, Serikali haioni kwamba kununua gari lake la maji ni bora zaidi kuliko kuendelea kukodi siku zote.
(c) Ni lini tatizo la maji litaisha angalau kwenye Manispaa ya Zanzibar.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 232 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali haikodi gari isipokua tunafanya katika njia ya kusaidiana, Serikali huwa inatia mafuta katika magari ambayo yanapeleka huduma hiyo kwa baadhi ya wananchi haja inapojitokeza.

(b) Kuhusu suala la ununuzi wa magari Serikali ilikuwa nayo magari yaliyokuwa yakitumika kwa kazi za usambazaji wa maji ili kuwasaidia wananchi wa baadhi ya maeneo. Magari hayo kwa sasa yamekongweka sana kiasi ambacho hayakubali tena matengenezo.

(c) Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar ina miradi mbali mbali ambayo inatekelezwa kwa misaada ya wahisani pamoja na nguvu za wananchi. Pia kutokana na jitihada za Wizara yangu tumefanikiwa kuibua Mradi mpya ambao unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) chini ya mpango wa (*ADF* 12) utakaobadilisha mabomba machakavu na kuimarisha mitandao ya Maji ya Mkoa wa Mjini/Magharibi. Miradi hiyo yote inayotarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2013 na inatarajiwa kupunguza tatizo la maji kwa kiasi kikubwa kama si kumalizika kabisa.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, kwa vile Mhe. Waziri amekiri kwamba magari yote ni mabovu na hayatengenezeki na ni mara ya pili kukiri hapa. Kwanza ulituambia kwamba ulikuwa na gari moja *crane* ni bovu na nikakujibu kuwa huna gari una sanamu. Je, serikali ina mpango gani wa kununua gari la maji ili wananchi wapate kuepukana na tatizo hili au unaliambia nini Baraza hili kuhusu kununua gari hilo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kuhusu suala la ununuzi wa magari kwa kweli ni suala muhimu na serikali imeliona hilo, kwa sababu tunajua ni jinsi gani wananchi wetu wanavyosumbuka hususan katika kipindi hiki. Kwa hivyo wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji tunategemea kununua magari mapya ya kusambazia maji pindi pale pesa tu zitakapopatikana.

**Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna baadhi ya sehemu nyingi hivi sasa zikiwem Sogea na Jang'ombe maeneo haya hawapati maji kwa muda mrefu hivi sasa. Je, Mhe. Waziri ni lini wananchi hawa watafaidika na huduma hii.

Je, ni lini Mhe. Naibu Waziri utawatembelea wananchi hawa wa Jang'ombe na Sogea ili kuwauliza matatizo yao haya, ahsante.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, ni kweli wananchi wa Jang'ombe na maeneo mengine kwamba wana upungufu wa maji na hilo serikali imeliona.

(a) Jitihada zetu ni kwamba tutajitahidi sana kuyashughulikia matatizo haya, kama vile tunavyoahidi kuyashughulikia matatizo mengine basi na hili *Inshaallah* tutajitahidi ili wananchi hao wafaidike nao katika suala hili.

(b) Mhe. Spika, kuhusu kuwatembelea wananchi wa Jang'ombe, suala hilo *Inshaallah* mimi niko tayari na wakati wowote pale nitakapohitajika. Namuomba Mhe. Mwakilishina Mhe. Mbunge, wanialike ili nije kutembea na safari hiyo niwe pamoja na wao.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, tatizo la maji bado limekuwa ni sugu katika Jimbo la Rahaleo na tunaelekea katika mwezi mtukufu wa Ramadhan. Je, Mhe. Waziri atahakikisha vipi kwamba tatizo la maji linaondoka katika Jimbo la Rahaleo katika kipindi hiki cha Ramadhan kinachokuja.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, ni kweli kipindi hiki cha Ramadhan ni kipindi kizito sana, hususan pale wananchi wanapokosa maji safi na salama. Lakini nimesema kwamba wizara yangu itajitahidi kusambaza maji kwa njia ya magari kwa baadhi ya yale maeneo ambayo yameathirika zaidi. Pamoja na kwamba hatuna magari, lakini tutatumia jitihada zetu kama zile ambazo tunatumia katika kipindi cha nyuma, kutafuta zile taasisi ambazo zina magari ili zituazime tutie mafuta na tupate kuwasaidia wananchi. *Inshaallah* tutajitahidi ili wananchi wapate kufanikiwa vizuri.

## HOJA ZA SERIKALI

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO KWA MWAKA 2011/2012

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Spika, kwanza kabisa nataka nitowe shukrani zangu za dhati kwako wewe mwenyewe kwa kuendesha vikao vyetu hivi kwa salama na amani hadi hii leo ambapo tunakaribia kuhitimisha bajeti yetu.

Pili Mhe. Spika, nataka niwashukuru Waheshimiwa Wawakilishi wote walioweza kuchangia, wamechangia kwa uwazi, ukweli na kwa mujibu wa demokrasia inavyowataka, nawashukuru sana. *(Makofi).*

Mhe. Spika, mimi nawaambia Waheshimiwa Wawakilishi kwamba yote muliochangia na muliyoniuliza nimeyasikia, nimeyafahamu na nimeyatafutia majibu na leo kwa kadiri ya uwezo wangu nitajitahidi kuyajibu.

Vile vile Mhe. Spika, napenda niweke kumbukumbu sahihi kuhusu masuala niliyoulizwa, mengine hayako katika wizara ambayo ninaisimamia. Mengine yameulizwa ni ya miaka ya nyuma. Lakini kwa sababu serikali ni endelevu na serikali ipo wanaoondoka ni wale wanaoongoza serikali. Kwa hivyo, nitajitahidi kuyajibu kwa kadri ya uwezo wangu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba niwataje wale wajumbe ambao walichangia hotuba ya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ni Waheshimiwa Wawakilishi 20, nikianza na:

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin — Mwenyekiti wa Kamati
2. Mhe. Rashid Seif Suleiman
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu

4. Mhe. Mussa Khamis Silima
5. Mhe. Hamza Hassan Juma
6. Mhe. Hija Hassan Hija
7. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
8. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
9. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
10. Mhe. Omar Ali Shehe
11. Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa
12. Mhe. Subeit Khamis Faki
13. Mhe. Ali Abdalla Ali
14. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
15. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
16. Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
17. Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi
18. Mhe. Ali Mzee Ali
19. Mhe. Fatma Mbarouk Said
20. Mhe. Mwanasheria Mkuu

Mhe. Spika, hoja zilizoulizwa ni nyingi na ninakiri kusema kwamba wajumbe wenzangu uliwapa muda wa kutosha kabisa, na mimi kwa heshima na taadhima nakuomba unipe muda wa kutosha kutoa ufafanuzi. Pale ambapo sikuwahi kutoa ufafanuzi si kwamba nimedharau ni kwa sababu zile za msingi nilizozieleza kuwa baadhi ya hoja tayari tumeshazipatia maamuzi na kwa mujibu wa Kanuni hatutakiwi tena kutafuta maamuzi. *(Makofi)*

Vile vile baadhi ya hoja ni za wizara nyengine si za wizara yangu.

Mhe. Spika, kwanza nataka nijibu ile hoja ambayo imetolewa na Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Hija Hassan Hija pamoja na Mhe. Ali Mzee Ali kuhusu uzaji wa mali za serikali kufuata utaratibu na sheria. Kwa kweli nataka nikubaliane nao kwamba mali ya serikali au mali yoyote ya umma kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi Waziri wa Fedha ana mamlaka ya kuuza mali ya serikali, lakini kwa utaratibu uliowekwa ndani ya sheria. *(Makofi)*

Nataka nikubaliane nao Waheshimiwa Wawakilishi kwamba lazima tufuate sheria katika kuuza mali za serikali. *(Makofi)*

Mimi kwa mamlaka aliyonipa Mhe. Rais pamoja na mamlaka niyopewa ndani ya sheria, basi nitahakikisha kwamba sheria inafuatwa na mali za serikali zinauzwa kwa mujibu wa taratibu na wala sitamuogopa mtendaji yeyote atakayevunja sheria. Mhe. Spika, suala hili nitalisimamia na ninakuombeni Waheshimiwa Wawakilishi tusaidiane katika hili. *(Makofi)*

Pili Mhe. Spika, ambalo limeulizwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin ni kuhusu Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani viimarishwe. Nataka nisema Mhe. Spika, Mkaguzi wa ndani ndiye anayemsaidia Katibu Mkuu ambaye ni afisa *responsible* wa wizara yake.

Kwa hivyo, unapokuja kuona kuna matatizo au ubadhirifu ama upotevu, basi ujue ni mambo matatu ya msingi yapo. Kwanza ni Mkaguzi wa Ndani yuko inafeciante, pili inawezekana kwamba Katibu Mkuu hasomi ripoti za Mkaguzi wa Ndani na hili nalo linawezekana ni tatizo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kuna haja na ninakubaliana na Mhe. Salmin Awadh Salim na hivi karibuni nimembatiza naye Mhe. Salmin Awadh Salmin sasa tutamitwa Dkt. Salmin. *(Makofi)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin nataka niseme kwamba tutaviimarisha vitengo hivi na tutawapatia mafunzo na miongozo Wakaguzi wa Ndani, ili waweze kusimamia vyema fedha za serikali. *(Makofi)*

Vile vile na mimi nitawashawishi sana Makatibu Wakuu kupitia Katibu Mkuu Kiongozi waweze kusoma ripoti za Wakaguzi wa Ndani pamoja na kushirikiana na Wakaguzi wa Ndani, kwa sababu pale ndipo wanapotambua matatizo na wanaweza kuyasahihishwa na kuyatambua. Kwa hivyo, mimi nakubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba hivi vitengo tutaviimarisha kupitia Mhasibu Mkuu. *(Makofi)*

Hoja nyengine Mhe. Spika, imeulizwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi na Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Asiye na Wizara Maalum) kuhusu utoaji wa mishahara ya watumishi wa serikali kupitia Benki ya Watu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nataka nithubutu kusema kwamba kila mtumishi wa serikali halazimishwi kufungua *account PBZ*, atafungua anapotaka mwenyewe na sio kwamba watumishi wote mishahara yao itapitia *PBZ*. Kwa hivyo, PBZ atapokea fedha kutoka serikalini kama ni mishahara ya watumishi halafu *PBZ* atazipeleka kwenye *account* za watumishi katika benki zao.

Lakini kwa wale ambao wameshafungua *account* zao *PBZ*, basi *PBZ* imejipanga vizuri. Mhe. Spika, nimeeleza kwamba tutafungua vituo vinne, Unguja viwili na Pemba viwili, kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa mishahara, hali kadhalika tutaongeza *ATM* tano mpaka 10, ili watu wetu wanapotaka kupokea mishahara yao wasiwe na matatizo.

Vile vile nimeshawagiza watendaji wa *PBZ* kuziangalia *ATM* kila wakati, ili kuona kwamba zinafanyakazi na kutoa huduma kikamilifu.

Mhe. Spika, hoja nyengine ambayo imeuliza na Mhe. Salmin Awadh Salmin na Mhe. Ismail Jussa Ladhu kuhusu mamlaka ya utoaji wa misamaha iwe kwa waziri anayesimamia masuala ya fedha. *(Makofi)*

Kwa kweli hili sina tatizo nalo na Mhe. Spika, utakumbuka siku za nyuma nililieleza hili na nikasema kwamba ziko sheria zinatoa mamlaka kwa mawaziri husika kutoa misamaha katika sekta husika. Hivyo, nimeshawaagiza watendaji wa *ZRB* kuzikagua sheria hizi zote na kuniletea, ili tuanze kuzifanyia marekebisho. *(Makofi)*

Hali kadhalika Mhe. Ismail Jussa Ladhu alieleza wazi na ninataka nikubaliana naye, kwamba kifungu cha 20 cha Sheria ya *ZIPA* hakitoi mamlaka ya moja kwa moja kwa *ZIPA* kutoa misamaha. Kwa hivyo, tutakiangalia kifungu hicho pamoja na Sheri nzima ya *ZIPA*, ili tuweze kuifanyia marekebisho na misamaha itolewe na Waziri anayeshughulikia masuala ya fedha. *(Makofi)*

Sasa kama kuna taasisi inahisi kwamba kuna haja ya kutoa misamaha katika eneo fulani, basi ni vyema wakamuomba Mhe. Waziri wa Fedha, ili naye akaliangalia kwa uzito wake na halafu akatoa idhini ya misamaha hiyo. Mhe. Spika, tutafanya hivyo na ninawashukuru sana walivyoliona hili suala, kwa sababu lengo letu ni kupunguza misamaha *as much as possible*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tutatoa misamaha kwa pale ambapo ni lazima tutoe misamaha na wala sio kila anayetaka kusamehewa basi asamehewe. Kwa hilo nakushukuruni sana Waheshimiwa na ninakuombeni sana tushirikiane na kila tutakapoiona sheria ina mwanya wa kutoa misamaha, kwa sababu sisi ndio tuliotunga ile sheria, basi tuweze kuirekebisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hoja nyengine iliyoulizwa na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mhe. Salmin Awadh Salim pamoja na Mhe. Ismail Jussa Ladhu kuhusu Ripoti ya *Joint Finance Commission*. Kwa kweli hapa nataka nimshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, kwa sababu ametoa ufafanuzi wa kina sana, yaani ameeleze SMZ tumeshatekeleza letu na kilichobakia wenzetu. *(Makofi)*

Lakini licha ya kwamba sisi tumeshatekeleza yetu, basi ninaimani kubwa sana na Serikali ya Mapinduzi inayoendeshwa na Mfumo wa Umoja wa Kitaifa, tutalisimamia ili na wenzetu na wao watoe maamuzi yao kwa faida ya muungano wetu.

Mhe. Spika, hoja nyengine iliyoulizwa na Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Hija Hassan Hija na bado nitaendelea kumwita mdogo wangu, kuhusu Idara ya Utawala na Huduma ina bilioni 9.76 na wametakujua mchanganuo ni kwa ajili ya matumizi gani?

Kwa hivyo, nataka niseme idara hii ndiyo inayowahudumia viongozi walioko madarakani kwa ajili ya safari zao za ndani na nje pamoja na wastaafu. Mhe. Spika, walioko madarakani ni viongozi watatu, yaani Mhe. Rais pamoja na Makamu wake wawili wanaposafiri kwenda Pemba, Dodoma na Ulaya, basi idara hii ndio inayotoa fedha kwa ajili ya kuwahudumia.

Sambamba na hilo tunao viongozi wastaafu wakiwemo Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, Mhe. Dkt. Salmin Amour Juma, Mhe. Dkt. Amani Abeid Karume na Mhe. Ali Hassan Mwinyi pamoja na Mawaziri Viongozi Wastaafu Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mhe. Dkt. Mohammed Gharib Bilali na Mhe. Ramadhani Haji Faki. Mhe. Spika, hawa wote wanahudumiwa na nataka nithubutu kusema katika mchanganuo wetu bilioni 4.491 ni kwa ajili ya safari. *(Makofi)*

Kwa hivyo, muone kwamba hizi fedha zilizowekwa hapa na nidhahiri kuwa fedha hizi lazima zikae hapa kwa sababu huwezi ikafika wakati Mhe. Rais, Mhe. Makamu wake pamoja na viongozi wastaafu wanataka kusafiri wizara yake husika itasema haina fedha na tutakamuliwa sisi Hazina tutoe fedha, kwa maana hiyo kwa umoja wetu tukasema kwamba hizi zikae hapa, ili Hazina wawahudumie viongozi wetu wanapotaka kusafiri.

Mhe. Spika, nimefarajika sana kuona kwamba viongozi wetu hawa wako kwenye *in safe hands* wanapotaka kusafiri kwa fedha zao kukaa hapa.

Mhe. Spika, hoja nyengine ambayo imeulizwa na Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Mussa Khamis Silima na Mhe. Hamza Hassan Juma kuhhusu kutoa kiwango cha asilimia ya kiwango cha mshahara wa chini kwa ajili ya kiwango cha chini cha pencheni. Kwa kweli nataka nithubutu kusema kwamba wazo ni zuri.

Mhe. Spika, hata mimi nilipokuwa Naibu Waziri wa Fedha kule Bara niliwaambia wenzangu kwamba tuangalieni kuwa na kiwango, yaani percentage cha mshahara wa chini iwe ndio kiwango cha chini ya pencheni, wazo hili ni zuri sana. Mhe. Spika, nataka nikubaliane na waheshimiwa waliotoa wazo hili.

Vile vile nataka nikuambieni kuwa faida yake hawa wazee kila gharama zinapoongezeka za maisha na kila tutakapokuwa tunapandisha mishahara, basi na wao pencheni zao zitakuwa zinapanda *automatic* bila ya matatizo. Lakini hasara yake au uzito wake ni kwamba huku nako gharama kwa upande wetu tutalazimika kutafuta fedha zaidi, kwa sababu kila unapoongeza mishahara *automatic* itabidi na hawa iongezeke.

Mhe. Spika, nataka niwaambie waheshimiwa wajumbe pamoja na wananchi kwa jumla wazo hili tunalifanyiakazi na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atakapotujaalia, basi tutaangalia uwezekano wa kuwa na kitu kama hiki na iitakuwa ni rahisi burdani na sio mamlaka tena ya Waziri wa Fedha kuja kusema 40,000/= au 50,000/=.

Hivyo, itakuwa tuna *formula* tumeshaiweka na tumeshakubaliana pia itampunguzia *headache* Waziri wa Fedha, kwani Waziri wa Fedha jamani amepewa mzigo mzito na huyu Waziri wa Fedha wa Zanzibar si Mnyamwezi kama mzigo mzito mpe Mnyamwezi. Kwa hivyo, mzigo huu ni mzito, lakini tukifanya maamuzi ya pamoja utaturahisishia sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, hoja nyengine ambayo imezungumzwa na Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na Mhe. Amina Iddi Mabrouk kuhusu wastaafu kupata usumbufu kwa ufuatiliaji fedha. Vile vile wengine wameeleza ni vyema tukawapa miezi sita na haya ni masuala mawili kwa pamoja, lakini nataka nijibu moja baada ya moja kwa ajili ya kutoa ufafanuzi.

Mhe. Spika, ni kweli hata mimi ninapokwenda Pemba kule nawaona wastaafu wale kwa kweli wanazifuatilia fedha mbali. Kwa mfano, anatoka Wete au Mkoani anajuka pale Chakechake. Kutokana na hali hiyo, tumeshakubaliana ndani ya ofisi kwamba tutaanzisha vituo, ili sisi tuwafuate wastaafu tutaweka *center* kwenye wilaya zetu, kwa ajili ya kuwa karibu zaidi na waweze kufaidika na pencheni zao badala ya kuitumia pencheni zao kwa nauli.

Lakini Mhe. Spika, nataka niseme tu ukianza kumpa mstaafu pencheni yake ya miezi sita ataitumia mwezi mmoja na halafu mwezi wa pili itakuwa ni usumbufu. Kwa mfano, tulijaribu kule Tanzania Bara, kwa kweli nililiona tatizo, sasa hapa walijaribu kutoa miezi miwili, kuwa wakati fulani walijaribu kutoa miezi miwili kwa ajili ya Sikukuu, basi ilipomalizika Funga ya Sita tu wengine wamesogea wanataka pencheni kumbe vile wameshaimaliza. Kwa hivyo, nadhani twendeni na utaratibu huu wa mwezi, lakini tusogeze huduma karibu na wastaafu.

Mhe. Spika, hoja nyengine iliyouliza na Mhe. Rashid Seif Suleiman alitaka kujua ni mikakati gani iliyopangwa katika kuongeza mapato kupitia Sekta ya Viwanda. Kwa kweli nataka niseme Mhe. Mjumbe Sekta ya Viwanda ni chachu ya mapato ya serikali na wala sio Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tu, serikali yoyote ile na lazima tuwe na mikakati katika kuimarisha viwanda, ili tuweze kupata mapato zaidi.

Mikakati ambayo tumeiweka ni hii ifuatayo:-

1. Kuhakikisha kwamba kila kiongozi kuanzia Mhe. Rais, Makamu, Mawaziri, Wawakilishi lazima tuwavutie wawekezaji wa ndani na nje wawekeze kwenye viwanda. Huo ni mkakati mmoja, yaani sote tunapokwenda na kurudi na kuonaa na wawekezaji wa ndani na nje, basi lazima tumvutie na kuwekeza katika viwanda.

2. Kufanya marekebisho katika Sheria ya *ZIPA* ni kutoa *incentives* zaidi kwa viwanda, kwa sababu huwezi viwanda hivi sasa *incentives* zake zifanane na *incentives* kwa ajili ya mahoteli haiwezekani. Kwa hivyo, huo ni mkakati wetu wa pili. *(Makofi)*

3. Kuziangalia sekta ambazo zinatoa matumaini makubwa tukazipa msukumo zikawekeza kwenye viwanda, moja ni Sekta ya Uvuvi lazima tuitizame. Taarifa nilizonazo hata tukiweka Viwanda Vitatu vya Uvuvi Zanzibar bado vitalishwa na rasilimali ilioko baharini.

   Kwa hivyo, mikakati hiyo lazima tuwe nayo kwa umoja wetu. Mhe. Spika, nimeshawishika sana kushirikiana na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, ili kwa umoja wetu tuje tuandae kama semina au mafunzo kwa Waheshimiwa Wawakilishi waweze kutusaidia katika ku-*sensitize* uwekezaji katika viwanda. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hoja nyengine ambayo imeuliza na Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Hamza Hassan Juma walitaka kujua vile vile bilioni 47.62 na bilioni 80.22 na bilioni 47.02 zote ni kwa ajili ya Wizara ya Fedha. Kwa hivyo, nataka nisema hapana.

Kwa kweli bilioni 47.62 hizi ziko Mfuko Mkuu wa Serikali na fedha hizi Mhe. Spika, tunalipia pencheni, viinua mgongo, deni la taifa mpaka matumizi ya dharura yanapotokea tunatoka kwenye mfuko huo, kwa hiyo hizi si za Wizara ya Fedha, isipokuwa hizi tumeziweka pale kwa matumizi yetu sote.

Kuhusu bilioni 47.02 ni fedha kwa ajili ya ruzuku kwa taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Fedha kama vile Chuo cha Fedha Chwaka, *ZRB*, Idara ya Takwimu, Mfuko wa Barabara pamoja na *ZIPA* zoe hizi tunazipatia ruzuku.

Vile vile Mhe. Spika, ilikuja hoja ya marekebisho ya mshahara 19.43 *billions*. Mhe. Spika, nataka niseme hapa na nawaomba Waheshimiwa Wajumbe mnisikilize kwa makini, kwa sababu tulitarajia zoezi la kufanyamarekebisho ya mishahara kukamilika hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011. Nasema kwa bahati mbaya wenzetu vikosi walichelewa wao. Kwa hivyo, majumuisho ya zoezi hili sasa ndio tunayafanya.

Hivyo, fedha hizi ni kwa ajili ya wizara zote na tukesha kupata kila wizara sasa mishahara mipya ni kiasi gani basi fedha hizi zitaanza kwenda kwa kila wizara, kwa sababu ilikuwa hatujakamilisha kwa kila wizara zilikuwa na ulazima wa kukaa hapa marekebisho na wala hakuna wizara nyengine yoyote itakayoweza kukaa nazo na halafu akawagaia wenziwe.

Lakini Wizara ya Fedha ndio *custodian* na halafu tukimaliza hayo majumuisho tunayapelekwa kwa wizara zinazohusika kwa ajili ya kufanya masahihisho katika sehemu zao za mishahara.

Bilioni 80.22 kama nilivyoeleza hizi ni fedha za maendeleo na wala si za Wizara ya Fedha. Mhe. Spika, kuna fedha hapa ambazo sisi tumetakiwa kuziweka tu pale na watumiaji ni wengine, hayo ni kwa mujibu wa makubaliano baina yetu sisi serikali na watoaji wa fedha hizo.

Kwa mfano, fedha hizi zinakwenda mpaka Mahakamani kwa Mwanasheria Mkuu, Wizara ya Ardhi, kwa *Government Registrar, ZIPA, Zanzibar Law Society, Urban Planning, Stone Town Authority* pia zinakwenda mpaka *Pemba Council* pamoja na ule Mradi wa *E-Government* bilioni 30, sehemu zote zinakwenda. Kwa hivyo, fedha zote zilizopo hapo ndio zimetengwa kwa ajili hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hoja nyengine ambayo iliulizwa na Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Subeit Khamis Faki kuhusu jengo la Pemba. Mhe. Spika, nataka nikubali kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein aliponitangaza kushika wizara hii nilifika Pemba, hata mimi nilisikitika nilipoliona lili jengo lilivyo. *(Makofi)*

Kutokana na hali ya jengo lile basi nilitafuta taarifa zake na nilipata taarifa na bado nikasema kwamba huyu mjenzi na *consultant* lazima tuwapeleke Mahakamani, sio tu kuwapeleka Mahakamani tunataka tupate chetu. Lakini ili tufike huko tukasema kwanza kama serikali basi tushauriane na Mwanasheria Mkuu, tuone jinsi tutakavyoweza kwenda.

Jengo hili Waheshimiwa Wajumbe walitaka kujua mpaka kukamilika kwake bajeti ilikuwa ni kiasi gani? Mhe. Spika, ilikuwa ni bilioni 1.45, lakini mpaka tumefikia pale tunataka kulisimamisha tulikuwa tumeshatoa nusu ya fedha hizo, lengo letu sisi ni kupata fedha zetu.

Kwa hivyo, tunamuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu katika hili atusaidie tupate fedha zetu, ili tuweze kufanya shughuli zetu za ujenzi katika maeneo au katika eneo jengine ambalo tayari tumeshalipata pale Chakechake. Vile vile wengine walitaka kujua kama tutajenga pale, kwa kweli pale hatujengi tena, kwa sababu tayari tumeshapata eneo jengine Chakechake na tutajenge jengo jengine Chakechake.

Mhe. Spika, pia wengine walitaka kuona mikataba. Nadhani hili Mhe. Mwanasheria Mkuu ameshalitolea ufafanuzi. Kwa hiyo, anayehitaji kuona mikataba ofisi yangu iko tayari kwa wakati wake muafaka, basi anaweza kuja kukaa na Mkurugenzi wangu wa Utawala na kuangalia na wala hatuna cha kuficha ndani ya mkataba ule. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hoja nyengine ambayo iliulizwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu, namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu ametoa ufafanuzi. Kwa kweli ilikuwa ni uhuru na nguvu katika kusimamia uchumi kwa upande wa Waziri wa Fedha wa SMZ. Mhe. Mwanasheria Mkuu hakubana maneno na wala mimi sibani maneno, tuna uhuru mdogo. *(Makofi)*

Sasa uhuru huu ni kwa sababu ya *design* ya Katiba, kwa sababu kuna mambo ndani ya Katiba ya kiuchumi anapaswa hivi sasa kutolewa na kila mmoja ashughulikie yake. Kwa hiyo, nadhani sisi Waheshimiwa Wawakilishi wa wananchi, basi tuwa-*sensitize* wananchi wetu katika kuchangia eneo hili yatolewe, ili kila mmoja ashughulikie la kwake kwa ajili ya kumpa uwezo Waziri wa Fedha wa Zanzibar aweze kusimamia masuala ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba uchumi wa Zanzibar ni uchumi wa visiwa, *is an Island economy*. Kuna wakati fulani Mhe. Spika, nilipokuwa Katibu Mkuu Wizara ya Mipango na Vitega Uchumi Mhe. Waziri wangu alikuwa Mhe. Ali Juma Shamuhuna kulikuwa kuna mkutano pale Mauritius *The Island Economy*. Kwa hivyo, sisi tulitakiwa tushiriki kwenye mkutano huo, lakini kwa bahati mbaya tukaongozwa na Mtagazwa aliyekuwa Waziri wa Nchi. *(Makofi)*

Sasa mambo kama yale kwa SMZ kwa Zanzibar hayatupi tija, kwa sababu *is an Island Economy Meeting*, leo naongozwa na mtu hatoki kwenye kisiwa, nasema kwa kweli Mhe. Spika kuna haja ya kuifanyia marekebisho na sisi tukaweza ku-*participate* katika maeneo ya kiuchumi wenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, swali jengine ambalo liliulizwa na Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Hamza Hassan Juma *is genuine question* walikuwa wanataka *clarification*, yaani ufafanuzi kuhusu *E-Government*. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe wanisikilize vizuri kwanza nataka niseme Mkongo wa Taifa katiak *design* ya awali ambayo inagharimu dola milioni 170 kutoka *Exim* cha China Zanzibar haimo, imekuja kusainiwa pale Dar-es-Salaam wakati mimi nilikuwa Naibu Waziri wa Fedha na Zanzibar haimo kwenye *design* ya awali, yaani Zanzibar haimo.

Kwa hivyo, tumepata mawasiliano kwamba Zanzibar itaingia katika *design* ya pili, sasa hiyo *design* ya pili kuombewa bado na wala hatujui itaombewa lini. Sasa wenzetu mwaka 2007 nimezungumza mengine ya zamani lakini nitaeleza kwa kadri ninavyoelewa. Mhe. Spika, wenzetu Baraza la Mapinduzi mwaka 2007 walisema aa! Sisi tuombe zetu kwa ajili ya kuandaa na sisi *E-Government* yetu.

Lakini ule mkongo ungepita hapa na sisi tungetaka kuunganisha basi tungeambia nyinyi hamna umiliki ndio yale tuyayasema masuala ya kiuchumi na tungeambiwa sasa mlipie. Kutokana na hali hiyo, tunaona ni vyema sisi tutayarishe ya kwetu na tuombe mkopo wa kwetu, ili tuwe na umiliki wetu.

Mhe. Spika, kwa sababu hii *E-Government* inawahusisha taasisi karibu zote na *Cabinet* ikafanya maamuzi kwamba Wizara ya Fedha usimamie ujenzi na mkisha kumaliza kusimamia ujenzi masuala ya kiufundi yatasimamiwa na Wizara ya Mawasiliano na masuala ya *operation*, yaani utumiaji yatasimamiwa na utumishi.

Kwa hivyo, mimi kazi yangu hapa nikesha kuujenga tu namuandikia barua Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano masuala ya kiufundi ni ya kwako na mimi nimeshanawa. Vile vile namuandikia Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kuutumia huo ni kazi yako na mimi nimemaliza, kama ambavyo Mhe. Ismail Jussa Ladhu ulivyosema ni sahihi kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Wizara ya Fedha haipaswi kuingia katika matumizi ya ule mkongo, yaani kusimamia matumizi na hiyo ni kazi ya Wizara ya Utumishi, kwa sababu Wizara ya Fedha haina utaalamu wa kuukarabati wa kuangalia ule mkongo unapotokewa na matatizo ni kazi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Kwa kweli kama alivyosema Mhe. Mwakilishi ni sahihi kabisa na hivyo ndivyo nitakavyofanya nikiwa naendelea ofisi hii. *(Makofi)*

Lakini nataka niseme *components* zake kama hivi ifuatavyo:-

(a) Tunajenga *Data Center* yake pamoja na *Saver* yake,

(b) Tutaunganisha sisi tunapochimba tunaunganisha kabisa katika majengo, yaani kuna baadhi ya wizara tutaanza kuziunganisha tutatoa *training* kwa watumishi watakaotumia hii, tutatoa *training* kwa mafundi na wataalam wa miundo mbinu ili hii iwe endelevu, bila ya *training* hapa haitakuwa endelevu. Lakini vile vile tuna *security* ambayo tutakayoiweka mkongo au hii *Government* yetu itakuwa ina *component* mbili kubwa.

Ya kwanza itatumiwa na seirkali lazima tuweke *security* taarifa zetu zisiweze kutoka na ya pili tunafanya mawasiliano sasa hivi na *ZANTEL* ili waendeshe kibiashara kule ili tuweze kupata mapato serikali, ni imani yetu kwamba tutakapofikia hatua hii mapato tutakayoyapata tutaanza kusahau shida za mapato lengo letu ni hilo kwamba huu uwe ni milki yetu ya Wazanzibari ndio maana tumekwenda tumechukua huo mkopo wa bilioni thalathini, naomba sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu na waheshimiwa wengine kwamba tukubali *ownership* hii iwe ni ya kwetu ili tusimamie vizuri kwa faida na manufaa ya wazanzibari. Vifaa vimekuja lakini kwa sababu kulikuwa kuna makubaliano ya mwaka 2007 tayari kulikuwa kuna makubaliano yaliyotiwa saini baina ya SMZ mjenzi na Serikali ya China vifaa vile tumevitoa na sasa hivi vipo katika *cast odium* yetu kwa sababu ni pesa zetu tumevitoa vile vifaa tumeviweka ili tuje tufanyie kazi.

Mhe. Spika, kulikuwa kuna hoja nyengine ambayo imeulizwa na Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Hija Hassan Hija walitaka kujua serikali ina wafanyakazi wangapi, na ile bilioni 19.4 nimeshaitolea ufafanuzi, katika idadi yetu ya watumishi wa umma tupo na 36,638.

Mhe. Spika, hoja nyengine ambayo nataka niseme hoja nzito iliulizwa na Mhe. Hamza Hassan Juma juu ya ukodishwaji wa hoteli ya *CLOVE INN* kama tunapata faida au hatupati faida, mkodishaji analipa au halipi hii hoja nzito. Kama nilivyosema nitasema kila ninalolijia sitalificha hoteli hii mategemeo yetu sivyo inavyokwenda, tulitegemea katika kipindi kifupi hoteli ilipe lakini haijilipi katika kipindi kifupi kulingana na *nature* ya shughuli za utalii Pemba, ndio kwa maana tukasema kwamba tufungue uwanja wa ndege ili tuongeze watalii Pemba, lakini vile vile aliyekodishwa anadaiwa dola 65 elfu, lakini nimefarajika tayari waliokodishwa na mkodishaji wameshatiliana makubaliano kwamba fedha hizo zitalipwa katika mwaka huu kwa awamu ndogo ndogo. Na mimi nitalifuatilia kuweza kuona fedha hizo zinalipwa hadi kukamilika kwake.

Mhe. Spika, hoja nyengine ambayo imeulizwa na Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Omar Ali shehe somu yangu ni hii ifuatayo. Huu utolewaji wa viwanja kkuna utamaduni sasa hivi viwanja vinakuwa vinamilikiwa na serikali halafu vinarejeshwa majenzi halafu vinatolewa, hapa kidogo nataka nitoe ufafanuzi tena waheshimiwa wawakilishi nataka tusikilizane ili tusije huko mbele tena tukaanza kuvutana vutana katika suala hili. Mhe. Spika, serikali inataka maendeleo *cast odium* wa ardhi ni Wizara ya Ardhi na anayetaka eneo kuomba hupitia wizara ya Ardhi, sisi tunaomba maeneo ya kujenga nyumba tunapewa tunaomba maeneo ya kujengea biashara zetu tunapewa kupitia Wizara ya Ardhi, unapokuta eneo liko wazi eneo lile linaweza kutumika kwa *development* alimradi hapa nataka ndugu zangu tufahamiane vizuri alimradi lisiwe limekuwa gazeti la serikali *that area is an space* haliwezi kutumika kwa *development* nyengine yoyote.

Lakini kama hujaligazeti eneo lile linaweza Waziri wa Ardhi akampa mtu aliyeomba omba mbele ya kiwanda cha maziwa Maruhubi zile *page* ndio mwisho wa kiwada cha maziwa mbele pale ni *open space*. Waziri mwenye dhamana ya ardhi ameona *for the development purpose* amelitoa eneo lile kwa kumpa muhusika kwa ajili ya maendeleo. Kwa hivyo ingekuwa eneo lile limekuwa *gazettes* lisingeweza kutolewa katika shughuli nyengine yoyote.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo lilikuja Mhe. Hamza alitaka kujua kwa nini *rest house* ya Pemba ya Wizara ya Fedha imeanza kulipwa mwaka 2009/2010 nataka niseme tu haya ndio mambo yale ya zamani niliyoyasema, lakini kwa sababu nimeyakuta na kwa sababu nimeulizwa nitayatarutia majibu nitajibu. Nyumba ile imejengwa mwaka 2004/2004 imejengwa na ikatiwa fanicha mjenzi hajalipwa pesa yake, mwaka 2009 mjenzi kaanza panda shuka, panda shuka. Serikali ikaiamuru Wizara ya Fedha kwamba andaeni *program* ya kumlipa mwezi mwezi mpaka mmalize deni, hali imeanza kulipwa mwaka 2009/2010 kwa sababu huko nyuma tumekaa muda mrefu hatujamlipa na ndio sababu tukaanza kumlipa.

Mhe. Spika, hoja nyengine imeulizwa na Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Mbarouk Mussa Wadi hisa za Zanzibar *BoT* hapa kidogo kuna hesabu na mimi naomba kidogo munistahamilie, wakati inavunjika *East African Clarence Board* Tanganyika ilikuwa ina paundi laki 666,667 na Zanzibar ilikuwa na paundi 84,000 kwa kumbu kumbu zetu sisi Zanzibar fedha hizo zimekwenda *BoT* zimechukuliwa na Muungano kwa kumbu kumbu zetu sisi zimekwenda kule. Sasa hii 84,000 ya jumla hii 750,667 ni asilimia 11.052 hiyo ndio asilimia sisi tunasema kwamba tuna hisa hizo nataka niishie hapo.

Lili kuja suala kwa nini tuna *account BoT* mtakumbuka *PBZ* nyuma ilikuwa na misuko suko tukaona bora *account* zetu tuzipeleke *BoT* lakini tumeweka *BoT* kwa sababu pale unapata udhamini wa kukopa kwenye masoko lakini hali kadhalika tunazo *account PBZ* , lakini pale pana usalama vile vile tofauti na hizi benki nyengine hizi benki nyengine hizi zikifilisika na wewe umefilisika pale *BoT* pana usalama vile vile. Kwa hivyo ni vizuri kwa serikali kuwa na *account* katika benki kuu serikali yoyote ile na *PBZ* tunayo *account* yetu.

Mhe. Spika, lilikuja suala je, tunapata gawio Mhe. Spika, nataka nikiri kwamba tokea mwaka 1994 serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunapata gawio kutoka *BoT* faida kwa asilimia 4.5 hapa ndipo tunapozozana, shea zetu sisi kwa mujibu wa kumbu kumbu zetu tunasema ni *eleven* nyinyi mnatupa gawio la 4.5. Hapa ndipo tunapokwenda na nashukuru Mhe. Hamza hili analijua vizuri sana kama ninavyoanza mimi kulijua sasa tutashirikiana na Mhe. Hamza Hassan Juma katika kufuatilia kufuata hizo kumbu kumbu ambazo yeye anazo.

Kuna suala jengine kwamba Mhe. Hamza Hassan Juma aliniomba wanafunzi wa Chwaka waruhusiwe kufanya mitihani, aliniomba nashukuru ndugu yangu mwenzangu rafiki yangu na mimi nataka niseme, ndugu yangu mwenzangu rafiki yangu hatukatazi wanafunzi wa Chwaka kufanya mitihani, lakini tunachokikataa ni kutoa *blanket* ukitoa *blanket* kila mwanafunzi aliyekuwa hana fedha akafanye mitihani wote watasema hawana fedha wakafanye mitihani. Tunasema kwamba kila mmoja ana kesi yake tofauti aandike barua yake aeleze kesi yake tutatathmini kesi moja baada ya moja tutakazoziona *genuine* tutawaruhusu wafanye mitihani na mimi nimeshawaelekeza tayari uongozi wa Chuo cha Chwaka kuanzia leo wanafunzi wapeleke barua zao waelekeze matatizo yao tutaangalia mmoja baada ya mmoja . Hatuna matatizo na hilo hawa wote wanaosoma pale ni vijana wetu ni ngugu zetu ni watoto wetu tunawataka waje watumikie nchi hii. Lakini wakati huo huo tusisahau Chuo hiki tunakipa ruzuku tu kinakusanya mapato kulingana na ada ili kiweze kujiendesha.

Mhe. Spika, hoja nyengine ambayo imeulizwa na Mhe. Hamza Hassan Juma imekuwaje tumemlipa Ali Yussuf mpaka deni la mwaka 2016 nataka nikiri, tumemlipa Sheikh Ali Yussuf deni lake mpaka la mwaka 2016 hatudai anatudai la mwaka 2017 tu, kwa nini tumefanya hivyo tumefanya hivyo baada ya kupata maombi ya Baraza lako tukufu kamati ya uongozi imetupa maombi kwamba jamani kuna matatizo ya kiuchumi jengo hili halitamalizika kama hatujamsaidia huyu, tumeweza na maombi yapo.

Hata juzi hii tunayozungumzia jengo kuvuja tumepata tena barua kueleza kwamba tusaidie kulipa *installment* ya mwaka 2016 ili atukarabatie jengo letu, ninachotaka kusema kila unapokuwa na uwezo ukalipa malipo ndio bora kwa sababu nimeshaona huku ukicheleweshe malipo ya watu watu wanakuja kukudai na riba, sasa mimi nasema ukiwa na uwezo na kwa sababu hili jengo leo tunalitumia tunafarajika sana kulitumia hili jengo mimi namshukuru sana Mhe. Hamza kwa hili kuliona hiyo *installments* moja iliyobakia nadhani tutaangalia mpaka mwaka 2017 lakini kwa maoni ya uongozi wa Baraza na hatuna utata katika hilo. Mimi nashukuru kwamba anagalau wameweza kupunguza deni hawajaniwekea kwenye kichwa mimi sasa hivi.

Mhe. Spika, kuna suala jengine liliulizwa hapa na Mhe. Hija Hassan Hija mdogo wangu anauliza Wizara ya Fedha ni ya nani, nataka nimwambie Wizara ya Fedha ni yetu sote mimi, wewe, wengine na wengine Wazanzibari hii ni yetu, na anayesema kwamba sisi hatumo hajui maana ya *public* hajui maana ya kuwatumikia wananchi hawa Mawaziri wanawatumikia wananchi na yale Mawizara yao ni kwa sababu ya kuwatumikia wananchi na Rais kawaweka pale kwa sababu ya kuwatumikia wananchi, wananchi yale ni majengo yao na Wizara yao kwa hivyo hii wizara yetu sote. Na wewe umo Mhe. Hija Hassan umo.

Mhe. Spika, wafanyakazi wa Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi Mipango ya Maendeleo hata sheria wanasoma nje Mhe. Hija Hassan Hija anasema hivyo, nataka nikuthibitishie tu Mhe. Hija Hassan Hija sina mfanyakazi wa Wizara yangu ambae amesoma sheria nje hivi sasa analipiwa nje hakuna, watu wangu wa sheria wote nimewatoa Tunguu nina mfanyakazi mmoja tu anasoma China na yeye yuko *under scholar ship* nina mfanyakazi mmoja amesoma Uingereza na nimemuajiri baada ya kurejea kusoma aliyempeleka Uingereza simjui, sina na mimi nina *discourage* sana sio wizara yangu tu lakini nina *discourage* wizara zote ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa nini tunapeleka nje wakati taasisi zetu zipo Bara na Zanzibar tena zinatoa *Quality* mimi nina *in carriage* sana Mawaziri na Makatibu Wakuu tupelekeni Tanzania tuanze na Zanzibar kama hatuna hapa tupelekeni Tanzania Bara, kwa hivyo Mhe. Hija Hassan Hija hilo usiwe na wasi wasi mimi nipo pamoja na wewe.

Serikali inanunua magari kwa vigezo gani Mhe. Hija Hassan Hija nataka nikwambie vigezo vipo na aina ya magari tunayotakiwa kununua yapo, magari makubwa tumeambiwa aina hii na magari madogo yapo aina hii hivyo vigezo vipo kama havifuatwi ni tatizo jengine na hili tutalazimika kulisimamia lakini vigezo vipo.

*ZSSF* ina mtaji kiasi gani Mhe. Hija Hassan Hija kauliza hili na somu yangu Mhe. Omara Ali Shehe kauliza hili nataka niseme tu *ZSSF* sio shirika hivyo haiwezi kuwa na mtaji, huu ni mfuko una thamani ya bilioni 73.06 thamani ya mfuko sio mtaji kwa sababu wao hizi pesa sio za kwao hizi ni zetu sisi tafouti na *PBZ* wao ni shirika na wana mtaji, huu ni mfuko sisi sote tumepeleka pesa zetu pale tumeweka kwa hivyo thamani ya mfuko ni 73.06 bilioni, kwa hivyo mimi naupongeza sana mfuko wetu kwa kuwa na thamani hiyo.

Suala jengine limeulizwa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwanza ndugu yangu nakupa pole nasikia hali yako leo kidogo si nzuri pole sana, yeye alitaka kujua kiwanja kiliopo karibu na Maktaba kuu ya zamani Vuga akasema Wizara ya Fedha tunavutana na mwenye kiwanja kile, nataka niseme tu lile eneo dogo lakini kuna viwanja viwili pale kimoja cha Wizara ya Fedha kimoja cha huyo mtu ambae Mhe. Mshimba amemzungumza nasikia wanaitwa jamaa zake kina Riami sijui kitu kama hicho, sisi Wizara tumemuomba lile eneo tupewe sisi na tuko kwenye mazungumzo kukubaliana kutokukubaliana na tumefanya vile kwa dhamira kwamba pale tupo karibu na Ikulu isingekuwa busara kukawa kuna *private building* nyingi tukasema kwamba *security purpose is much better* tuka *own* sisi serikali eneo lile. Mazungumzo yanaendelea tukifikia muafaka basi nitakuja kukunong'oneza Mhe. Mshimba tulipofikia.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk vile vile alisema kodi kwa watumishi wa shirika la umeme ni kubwa nataka niseme serikali imefanya maamuzi ya *consolidate* mishahara na maposho tokea mwaka 2007/2008 lakini kuna baadhi ya mashirika yalikuwa bado, Shirika la Umeme limefanya kazi hiyo sasa hivi lakini kiwango cha kodi ni ile ile sawa sawa na watumishi wengine lakini kwa sababu yale maposho yalikuwa hayakatwi kodi walikuwa wanapata mengi, sasa yameunganishwa na mishahara ndio hilo ambalo analiona hivi sasa. Lakini hii tumeifanya kwa sababu tu watumishi wengine wa serikali kuu tayari wameshafanya tumesema na mashirika nayo tuende huko ili kila mmoja tuwe tuna *fair play.*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk amesema kuwaelimisha wananchi juu ya kufanya biashara nakubaliana na wewe kabisa lazima tuwaelimishe wananchi wetu juu ya kuingia katika kufanya biashara, tutawaelimisha kupitia vyombo vya habari tutawaelimisha kupitia *training*, tutawaelimisha kupitia Wizara ya Ajira na Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi bila ya kuelimisha hawa wananchi wetu hawataweza kufanya biashara na ukishindwa kufanya biashara maana yake huwezi kuingia kwenye soko, soko la Zanzibar ni dogo lakini sasa hivi tuna soko la Afrika ya Mashariki, tuna soko la *SADC* utaingiaje huko kama huna elimu ya biashara. Kwa hivyo nakushukuru sana Mhe. Makame Mshimba hilo nitalisimamia ili tuweze kuwaelimisha wananchi wetu kwa faida ya nchi yetu.

Mhe. Spika, jengine ambalo liliulizwa na Mhe. Makame Mshimba na Mhe. Moh'd Mbwana walisema kwamba sheria ya *ZSSF* ifanyiwe mapitio ili kuruhusu kutoa mikopo kwa wanaochangia, sheria tutaifanyia mapitio na tukikamilisha vizuri vikao vyetu nimepanga na wenzangu mwezi wa oktoba tuilete kwa marekebisho. Lakin suala la kutoa mikopo *actuary study* ambayo imefanywa na wataalam wa *World Bank* wamesema, wameiambia *ZSSF* msifanye kazi mbili kwa mpigo wacheni mabenki yakopeshe nyinyi mutoe dhamana fedha yake aliyochangia iwe ni dhamana kwa maana walikuwa wanatahadharisha mfuko usije ukaanguka, tayari tumeshazungumza na mabenki na mabenki tayari yana mwelekeo wa kutukubalia kwamba watapewa mikopo kwa dhamana ya fedha zao ambazo wanaweka pale katika mfuko. Kwa hivyo hili nadhani litawasaidia sana wananchi wetu kuweza kutumia fedha zao kama ni dhamana kwa kupatia mikopo.

Sheria ya *ZIPA* ifanyiwe mapitio Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na Mhe. Ismail Jussa Ladhu nataka nithubutu kusema kwamba nayo vilevile tumepanga kuileta mwezi wa Oktoba kama mipango yetu yote itakuwa sahihi ili tuifanyie marekebisho.

Suala jengine ambalo Mhe. Mbarouk Wadi Mussa alitaka kujua Mhe. Spika, *BOT* na bodi ya *BOT na TRA* ina Wazanzibari wangapi, Bodi ya *BOT* ina wajumbe 9 Wazanzibari watatu. Bodi ya *TRA* ina wajumbe 13 Wazanzibari wawili na hakuna chombo hata kimoja katika hivi kilichowahi kuongozwa na Mzanzibari, alitaka kujua hakuna Wazanzibari wenye sifa tupo wengi tu mimi mmoja, Mtando wa pili, Maalim Haroun wa tatu tupo wenye sifa. Lakini haya ndio yale ambayo nimeyazungumza mfumo wetu tuwashajihishe wananchi wetu kuweza kurekebisha katiba.

Mhe. Spika, suala jengine taasisi zilizokaguliwa na Uhakiki mali Mhe. Mbarouk Wadi Mussa alisema mbona chache ni kweli lakini kazi inaendelea, wameanza kukagua zile lakini watakagua nyengine mpaka taasisi zote tumalize. Akasema katika idara yenye matatizo ni Idara ya Uhakiki Mali nataka nikubaliane na wewe kabisa na mimi kwa upya wangu sasa hivi nayasoma matatizo yao na namuomba Mhe. Mbarou Wadi Mussa tuendelee kushirikiana kila utakapona tatizo ili tuweze kuwasaidia kama tatizo lao kubwa ni mafunzo tuweze kuwapa mafunzo, kama tatizo lao kubwa ni uwajibikaji basi tuwaambie mnatakiwa muwajibike katika maeneo haya na haya. *All kip may ice* kwenye Idara hii ili nihakikishe sasa wanafanya kazi kwa speed ninayoitaka mimi.

Suala jengine Mhe. Spika, Mhe. Mbarouk Mussa Wadi alitaka kujua jengo la Mambo Msiige kuondoshwa katika milki ya serikali kwenda katika milki ya mtu, nataka nikwambie tu ndugu yangu Mhe. Mbarouk jengo bado ni letu wala hatulipeleki katika miliki ya mtu tutampa mtu atumie tu lakini jengo ni la serikali na litaendelea kubakia kuwa jengo la serikali.

Kuna suala jengine la Mhe. Mwejuma Faki Mdachi tatizo la ofisi ya Shirika la Bima Pemba nataka nikubaliane na wewe Mheshimiwa mimi mwenyewe nimetembelea ofisi ile, nimeona kuna kijichumba kidogo anakaa masikini wafanyakazi nikamuulize yule mama nikaambiwa ni msimamizi pale akanambia Mheshimi ndio ofisi yatu hii. Lakini nataka niseme hali halisi kwa taasisi zetu zote ilikuwa hivyo kwa sababu tulikuwa hatujaamka kujenga majengo ya ofisi, sasa ndio tunaamka nataka kukuhakikishia Mheshimiwa Muwakilishi tayari Bima tumeshapata kiwanda Chake Chake tukimaliza Jengo la Zanzibar nimesema litamalizwa Septemba tutaanza hatua za michoro kwa ajili ya jengo la Pemba la Bima.

Mhe. Spika, kuna suala jengine ambalo limeulizwa na Mhe. Omar Ali Shehe na Mhe. Hija Hassan Hija mikakati ya kukusanya mapato na kuzuia uvujaji, nataka niwashukuru sana hawa ndugu zangu tuna mikakati mizito sasa hivi ya kuangalia jinsi gani mapato haya tutaweza kuyakusanya kwa ukamilifu na jinsi ya kuzuia uvujaji kuna *entry point* mbili *Air Port na* Bandarini tumeanza pale. Lakini ukianza sasa hivi kuitangaza mikakati yako ya kuzuia mapato wajanja nao wanakusikiliza wataandaa *counter* sasa nataka kwanza niachieni nifanye mikakati yangu halafu baadae tuone kama itafeli. Lakini lengo letu ni kuhakikisha kwamba mapato yote yanakusanywa na uvujaji haupo sio unapungua lakini haupo, kwa wale ambao watachota mapato ya serikali basi sheria ichukue mkondo wake.

Mhe. Spika, Mhe. Omar Ali Shehe alisema sheria ya fedha ina mapungufu nataka nikubaliane na wewe tutaipitia sheria ya fedha tuone mapungufu yako katika maeneo gani na kwa sababu baraza letu liko *active* tutaileta barazani tutakapokamilisha ili tuweze kuifanyia marekebisho.

Mhe. Omar Ali Shehe vile vile aliuliza kwamba kuchapisha risiti za serikali nje ya *press* nataka nikubaliane nae kweli hivyo ndivyo tunavyofanya, lakini kuna sababu tunachapisha risiti nje ya serikali kwa sababu risiti zetu zina *security fictures* na *press* bado hawajawa na utaalam huo, tumeongeza na wenzangu tuangalie jinsi ya kuiwezesha *press* iweze kuwaka hizo *security ficture* katika risiti badala ya kuchapisha nje basi ziweze kuchapishwa pale *press*. Sasa hivi kama utakumbuka katika hotuba ya Makamo wa Pili wa Rais ameeleza kwamba *press* sasa tunataka kuisadia kuijenga ili iweze kufanya kazi vizuri zaidi na mimi nitakuwa karibu sana na Mhe. Omar Ali Shehe ili tuhakikishe kwamba hizi risiti basi hatimae tunazichapisha kwenye *press* ya serikali.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo Mhe. Omar Ali Shehe amateka kujua au ameniomba Kamati ya *PAC* iwezeshwe ili iweze kuchambua bajeti, nataka niseme yafuatayo tumeanza vizuri sana na nataka niunganishe sio kamati ya *PAC* peke yake hata kamati ya Fedha tutazipatia uwezo huo, tutazipa mafunzo mafupi ili waweze kuchambua vizuri bajeti zetu za serikali. Hilo ndio lengo letu, wawakilishi waweze kuzichambua bajeti zetu.

Mhe. Omar Ali Shehe aliuliza vile vile, alitaka ufafanuzi wa ziada juu ya mradi wa Zanstat kwamba mradi huu una ufadhili wa *Africa Capacity Building Foundation*. Kazi yake kubwa ni ku – *strengthen statistical activities* kazi za takwimu kwa kuwapatia mafunzo wa takwimu, kwa kuwapatia vitendea kazi kwa maana kompyuta na vitendea kazi vyengine pamoja na magari. Ndio mradi huu ambao fedha zake zinatoka katika *Africa Capacity Building Foundation*. Sasa hivi Idara yetu ya Takwimu ukiwatembelea wana kompyuta za kutosha, wana magari afadhali na wengi tayari wameshapata *training* katika wafanyakazi wetu wa Idara ya Takwimu. Ndio mradi huu majukumu yake.

Mhe. Mahmoud Muhammed Shemeji yangu, alitaka kujua taratibu za uajiri TRA. Uajiri ndani ya TRA ni *open market*, kama kuna nafasi TRA ipo Zanzibar au ipo Bara inatangazwa na inategemea sifa za muuombaji, uki – *qualify* unaweza ukafanya kazi Bara au unaweza ukafanya kazi Zanzibar. Lakini suala hili nafasi za Muungano kwa Wazanzibari limeanza kujadiliwa na Wizara zetu mbili, Utumishi Muungano na Utumishi Zanzibar. Ili Wazanzibari waweze kuwa na nafasi zao maalum katika utumishi wa Muungano.

Suala jengine limeulizwa na Mhe. Subeit Khamis, ametaka kujua PBZ iliyofunguliwa Muzamil nilieleza ni kwa ajili ya wateja wakubwa. Vigezo vyake alitaka kujua ni nini. Kituo kile kuna wateja wakubwa ambao wanapokwenda kuweka pesa pale wanakwenda na mabegi ya pesa. Sasa unapomuhudumia yule mmoja hawa wengine wadogo wadogo wanaweza wakakaa sana. Tukasema hetu tutengeni kile wao waende huku, hawa wadogo wadogo wahudumiwe. Maana ukenda wewe *counter* anahudumiwa mtu unamkuta yule mtu wa *counter* anamuhesabia milioni 500 ni lazima Benki wasihesabu, wale wadogo wadogo watakaa kutwa wale. Lakini kituo kile hakimkatazi mteja mdogo mdogo kwenda. Lakini wale wakubwa tumewapa nafasi waende huko. Hilo ndio lengo letu.

Hapa kwetu kiwango cha mteja mkubwa unakijua kama una milioni 100 unaweza ukenda zako kule, Mhe. Subeti unakaribishwa. Kwa wenzetu vituo kama vile ukiingia mteja mkubwa unawekewa na kikombe cha kahawa, huku unakunywa kahawa huku unafanyiwa kazi yako. Na sisi tumefanya hayo mapinduzi sasa hivi tunakwenda na wakati.
Mhe. Spika, Mhe. Subeti alikuwa anataka kujua jengo la ZRB gharama yake. Nataka niseme tumeanza vizuri kujenga majengo ya serikali. Muda mrefu sana tumekaa katika majengo ya Mji Mkongwe. Sasa hivi majengo yale yanahatarisha hata usalama wa wafanyakazi wetu. Jengo la Kilimo limeshadata mara mbili Fodhani, kwa bahati wafanyakazi wetu wanaofanya kazi katika majengo haya wana mbio. Maana yake tunapokuwa mashuleni kule *primary* tunafundishwa kwenda *cross country*. Lakini yale majengo sasa hivi hali yake si nzuri, *move* ya kujenga majengo mapya yatatujengea heshma Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hivyo jengo hili mpaka sasa tumeshatumia bilioni 5.9 na mpaka litakapokamilika kwake tutatumia bilioni 7.2. Lakini *is a very beautiful building.*
Mhe. Spika, namalizia bado kidogo tu. Mhe. Ali Abdalla Ali na Mhe. Amina Iddi wametaka mfuko wa barabara kuendeleza barabara katika maeneo yao, Mhe. Ali kasema Mfenesini.

Nataka niseme huu mfuko wa barabara haujengi barabara, wao wanadhamini ujenzi wa barabara. Wao wanahela halafu wanamtafuta mjenzi wanamwambia tujengee barabara hiyo. Hawa hawajengi barabara kwa mujibu wa sheria yao inayozidi kilomita moja, wao wanakarabati barabara. Zile barabara za kukarabatiwa nimezipokea na tayari nimeshaongea na mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Barabara, aangalie hizo barabara zilizotajwa. Kwa upande wa Mfenesini nitaongea na Waziri wa Miundombinu alete watu aangalie jinsi tutakavyoweza kudizaini ujenzi katika maeneo hayo. Tutashirikiana na Waziri wa Miundombinu.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Abdalla amesema mfuko uwekeze Tanzania Bara. Uwezekano upo, tutaangalia. Amesema PBZ waende Mwanza na Arusha, nakubaliana na wewe. Maeneo haya yana *potation*. Bima ipo Arusha inafanya vizuri, naamini na PBZ akenda Arusha watafanya vizuri.
Mhe. Ali Abdalla ameuliza tunajiandaaje katika Bima ya Afya kwa watumishi wetu. Hapa nataka niseme mambo mawili.
Kwanza utafiti unaendelea kuona *how far can start* bima ya afya. Lakini vile vile tutakuwa tuna maamuzi ya kufanya baadaye. Aidha tuanzishe mfuko wa Bima ya Afya au tuwaruhusu watu wetu kutumia mashirika ya Bima yaliopo kwa ajili ya afya zao. Tutaangalia baadaye lipi ni bora zaidi kwa upande wa watumishi wetu. Lakini wazo ulilolizungumza ni zuri na mimi tokea nimeingia nimezungumza na wenzangu wa Bima tunaliangalia hili suala. Mhe. Ali Abdalla alitaka kujua mwaka 2010/2011 misaada tuliyoipata ni kiasi gani. Tumepata misaada ya bilioni 136.67 bilioni 84.764 ni mikopo na bioni 51.91 ni ruzuku.

Mhe. Amina amesema SMZ Dar-es-Salaam nafasi ni ndogo na watendaji. Nataka niseme mimi jana nimewauliza, kwa sababu kila nikenda kwenye ofisi ile zaidi ya mara ya kwanza niliyotembea nikaliona lile jengo, nikenda nakwenda kwenye ofisi yangu nakaa nafanya kazi zangu. Nimewauliza wenyeji Ofisi ni ndogo wamenambia wao ofisi ile inawatosha na kuna baadhi ya vyumba bado hawajavitumia.

Lakini vile vile watendaji tuliowapeleka pale licha ya kwamba kuna ukweli baadhi yao walikwenda kwa sababu ya kuolewa, lakini wanasifa zao, yaani wamekwenda pale wanauwezo wa kufanya yale majukumu yao. Kwa hivyo najua wapo wengine wamepelekwa pale waume zao wapo kule. Lakini wana sifa za kufanya kazi katika yale maeneo tuliyowapangia. Vyenginevyo tusingeweza kuwapangia maeneo yale. Lakini bado nakubaliana na Mhe. Amina kwamba watendaji wa SMZ wanahitaji kupewa mafunzo zaidi ili waweze kufanya kazi kwa ubora zaidi.

Mhe. Mohammed Mbwana ametaka kujua fedha za uuzaji wa Meli ya Mapinduzi ni kiasi gani na ziko wapi. Mimi namshukuru sana kaka angu Mhe. Ali Mzee Ali. Ametoa ufafanuzi mustakabali wa meli mpaka ulivyokwenda mpaka ilipouzwa. Wakati huo mimi sikuwepo. Lakini nataka niseme meli ile imeuzwa kwa dola laki 410 na fedha zake zipo Hazina zimewekwa, tunasubiri maelekezo ya serikali.

Lakini kulikuwa hakuna *solution* kama alivyosema Mhe. Ali Mzee, aidha mliuze au mkate *scraper*. Lile meli lilikuwa limeshakwisha. Wengine mlisikia lilikuwa linakwenda zake zijui pahali gani limekanyaga mwani huko likatoboka. Hii inaonesha dhahiri kwamba zile meli zime zilikuwa zimeshakwisha. Serikali ililazimika kuziuza na ninalo faili zima hapa, wamefata taratibu zote mpaka wameliuza.

Mimi nataka niseme kwamba maelekeza ambayo Mhe. Waziri wa Miundombinu ametoa kwamba tuna mpango wa kuangalia uwezekano wa kununua meli nyengine na yale ambayo amesema bwana Ali Mzee, nunua meli Waziri wa Fedha. Serikali tumelisikia, tumelipokea na tutalifanyia kazi.
Mhe. Mohammed Mbwana alitaka nimpe orodha ya mali iliyokodishwa na Idara ya Uhakiki Mali kwa miaka 99. Idara ya Uhakiki Mali hawana kitu chochote walichokikodisha kwa miaka 99. Wao wanakodisha miaka mitano, kumi tena wana *review* mengine mitano, kumi wana *review*.

Lakini kama nilivyosema kuna baadhi ya maswali niliyoulizwa sio ya kwangu. Ardhi wanao uwezo huo wa kukodisha miaka 99 na tumewapa sisi kwa mujibu wa sheria na taratibu zetu. Lakini mali ya serikali kukodishwa miaka 99 sijui kama kuna kiwanda kinakodishwa miaka 99 uwezo huo hawana. Kwa hivyo sina orodha hiyo. Kama yeye mwenzangu anayo orodha hiyo basi namuomba tushee hiyo orodha na mimi niweze kufaidika.

Mashirika ya umma kufanyiwa tasmini. Mhe. Ali Mzee na Mhe. Haji Faki Shaali. Nataka nikubaliane na nyinyi, mashirika ya Umma haya tuna mashirika ya Umma manane, ukiacha PBZ kama nilivyosema mwanzo. Mashirika yote yanasuasua tu, ni lazima tufanyie tathmini tena tathmini kubwa kama tulivyoifanyia PBZ ili yaweze kufanya kazi. Vyenginevyo haya mashirika yatakuwa yanaendelea kututia hasara tu. Mashirika haya hayachangii chochote serikalini. Mengine yanatafuta ruzuku kutoka serikali wapewe wao. Sasa si bora ikaitwa idara.

Nasema kwamba namshukuru sana Mhe. Ali Mzee na Mhe. Haji Faki Shaali tutayapitia mashirika haya kwa pamoja, ikiwezekana hata kutafuta wataalamu wa kutusaidia ili tuyafanyie *restructure* ili yaweze kufanya kazi.
Mwisho Mhe. Spika, suala ambalo limeulizwa na Mhe. Fatma Mbarouk. Maslahi ya wafanyakazi bado ni madogo ingawa yanaongezeka. Nataka nikubaliane na wewe. Kwa nini ni madogo?

Ni madogo kwa sababu hali yetu ya uchumi ambayo inachangia mapato ya serikali bado ni ndogo. Tukiimarisha uchumi mapato yetu yataongezeka nadhani maslahi itakuwa tunayaongeza. Kama alivyosema Mhe. Rais na mimi nataka ninukuu.

"…tutaongeza maslahi ya watumishi kila hali yetu ya uchumi itakapokuwa nzuri"

Mhe. Spika, nataka nimalizie kwa kuwashukuru sana waheshimiwa wawakilishi kwa maswali yao. Nataka niseme tu, nimejitahidi kwa sababu mengine yalikuwa ni ya zamani nimelazimika kwenda kusoma, jana nimelala saa 6:00 ya usiku kwa kusoma, nimelazimika kuyasoma na kuyafahamu ili nije niwasaidie waheshimiwa wawakilishi.

Nina imani kwamba nimekusaidieni waheshimiwa na kama kuna swali ambalo mnahisi kwamba sijakupeni ufafanuzi mzuri muda tunao, mimi nipo, ofisi yangu ipo wazi, niko tayari kushirikiana na nyinyi.
Mhe. Naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi, Mipango ya Maendelea:** Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza lako limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya Matumizi vya Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

**KAMATI YA MATUMIZI**
**Makadiri ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa Mwaka 2011/2012**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0201 | Idara ya Forodha | 1,580,910,000 |
| Kifungu 0401 | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 2,785,999,000 |
| Kifungu 0701 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 51,680,000,000 |
| Kifungu 1301 | Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma | 340,000,000 |
| Kifungu 1801 | Bodi ya Mapato Tawi la Pemba | 5,818,560,000 |
| Kifungu 2203 | Bodi ya Mapato Afisi Kuu | 103,825,491,000 |
| **Jumla ya Fungu** | | **265,030,960,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 19 – AFISI YA RAIS FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0301 | Afifi Kuu Pemba | 716,263,000 |
| Kifungu 0401 | Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | |

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii kuweza kuchangia baadhi ya mambo.
Mhe. Spika, nilipokuwa nimeuliza swali langu kuhusu JFC Mhe. Waziri alikuja kujibu hapa lakini majibu yake yakawa hayajanitosha. Pamoja na ufafanuzi ulikuwa umetolewa na Mwanasheria Mkuu lakini bado sijafaidika na majawabu ambayo nimepata.

Hapa nina hansard zenye hotuba za viongozi hawa wawili Waziri wa Fedha wa Bara na Waziri wa Fedha wa Zanzibar. Labda nianze na Waziri wa Fedha wa Zanzibar.

nasema kwamba tume ya pamoja ya fedha serikali inaendelea na juhudi za kushirikiana na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa mapendekezo juu ya taarifa ya Tume hiyo yaliyowasilishwa katika Serikali zote mbili.
Hapa katika jawabu Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Waziri walijibu kwamba:

> "Kwa upande wetu Zanzibar tumeshamaliza, tunawasubiri wenzetu wa Bara ili wao waweze kutupa taarifa au waweze kutoa na wao mapendekezo yao, ili tuweze kuja kukaa pamoja na kutoa muafaka wa suala hili."

Hili suala kama unavyolielewa Mhe. Spika, sasa ni muda mrefu mno. Lakini taarifa ya Waziri wa Fedha wa Tanzania inasema kama hivi ifuatavyo:

> "Kila upande unaendelea kufanya uchunguzi wa mapendekezo ya tume na kuwasilisha maoni yake katika kikao cha pamoja"

Mhe. Spika, kikao hichi kitakuwa lini na hili suala bado wakati linaleta utata sana katika masuala yetu haya ya maendeleo na uchumi wa nchi yetu. Tunaomba taarifa ya ziada kutoka kwa waziri atwambii hasa hichi kikao au kitu gani hasa kinachosababisha matatizo haya.

Lakini pamoja na yote hayo wakati tupo katika kamati zetu, tulimuomba Mhe. Waziri tufanye utaratibu wa kukutana Kamati yetu ya Fedha na Uchumi pamoja na ile ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ili tuhakikishe kwamba tatizo hili linafikiwa ufumbuzi na kumaliza matatizo yaliyopo. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Spika, ni kweli nataka nimshukuru Mhe. Mwakilishi, katika hili. Labda niseme tu Mhe. Spika, katika ripoti ile kuna mambo mawili ya msingi. Jambo la kwanza ni kufungua *account* ya pamoja. Tutaifunguaje hiyo *account* ya pamoja ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari imeshatoa mapendekezo yake.

Jambo la pili jinsi tutakavyoweza kuichangia hiyo *account* ya pamoja. Tayari Serikali ya Mapinduzi imeshatoa mapendekezo yake. Tunachokisubiri sisi wao Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania wamalize mapendekezo yao. Halafu mapendekezo haya yanakuja katika kamati ya pamoja, wao hawajamaliza mapendekezo yao. Sisi kama Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hatuwezi tukaya *expose* mapendekezo yetu. Lazima mapendekezo yetu tuyafiche sisi wenyewe. Tunataka twenye katika Kamati ya Pamoja, someni yenu na nyinyi someni yenu, tunasoma pale pale kila mmoja anayasikia ya mwenzake pale, tunaanza kuyachambua kwa pamoja.

Mimi nataka nimwambie Mheshimiwa kwamba tunasubiri sana kikao cha Makamo wa Rais. Kikao cha Makamo wa Rais kitakapoitishwa, kilipangiwa tarehe kiitishwe lakini nakumbuka Makamo wa Rais alikuwa na dharura kikaahirishwa nasikia alikwenda Mkutanoni New-York. Lakini sasa tunasubiri kikao tena chengine. Na kwa sababu mratibu wetu ni Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais nadhani atawasukuma wenzetu waandaa hicho kikao katika muda huu mfupi kiweze kuitishwa ili tuweze kulikamilisha hili suala.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri labda niseme tu kwamba miaka mitano imeshakatika, tunaendelea kumuachia tena kwa mwaka huu umalizike na mwaka unaofuata suala hili nitalirejesha tena labda itakuwa tumefikia pahala ambapo itakuwa kwa Wazanzibari na Watanzania italeta manufaa zaidi. *Ishallah,* tuendelee.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza nimpongeze sana Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kuwa muwazi na fasaha katika maeneo mengi ambayo tumemuuliza na tungekuwa tunakwenda namna kama hii kama nilivyosemka juzi tulivyokuwa tunapitisha Wizara ya Biashara na Masoko nadhani hata maswali yangelikuwa yanapungua sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu zipo hoja mbili ambazo nilikuwa nikitaka ufafanuzi. Lakini ili kuwapa nafasi na wenzangu mimi naomba nishike moja tu. Hili ni suala zima la *E-Government.* Katika majibu yake Mhe. Waziri kwanza katoa ufafanuzi kuhusu suala zima la ule umradikuwa ulikuwa unafadhiliwa katika mkopo ambao ungejumuisha Jamuhuri nzima ya Muungano na akasema Zanzibar inaingizwa katika *phase II.*

Pili akasema wizara yake imelichukua hili kwa sababu ya maamuzi ya Baraza la Mapinduzi kwamba ilisimamie suala zima la ujenzi. Sasa nataka nianze hapa Mhe. Mwenyekiti.

Kwanza hapa sisi tunajadili makadirio yanayoletwa na serikali kwa hivyo serikali inawajibika kwa ujumla wake. Kwa hiyo hata hayo maamuzi ya Baraza la Mapinduzi, Baraza hili linao uwezo wa kuliagiza Baraza la Mapinduzi kwamba liyabadilishe.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba mradi wa *E– Government* kwa maumbile yale na kwa alivyousema mwenyewe na kakubaliana na mimi ulipaswa uwepo katika Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu. Sasa ningelifahamu kama angelinambia kama alivyotoa ufafanuzi katika miradi mengine kwamba zile fedha ambazo zipo katika Wizara ya Fedha zimewekwa pale kama dhamana. Lakini utekelezaji wa mradi ule unakwenda katika wizara inayohusika. Lakini hapa katwambia ujenzi wenyewe wa mradi umewekwa chini ya Wizara yake. Ukisoma kitabu chake Mhe. Mwenyekiti ukurasa wa 39 unasema.

> "Kusimamia utekelezaji wa mradi wa *E-Government"*

Mhe. Mwenyekiti, hapa ninavyo vitabu vitatu ukijumlisha na chake yeye vitakuwa vine. Suala hili kila mtu anaonekana analitaja taja. Ukija katika hotuba ya Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora anazungumzia *E-Government*, ukizungumzia hotuba ya Mawasiliano wanazungumzia suala hilo. Hili naomba Mhe. Mwenyekiti tusaidiane ili tuweke maamuzi sahihi kabla hatujapitisha fungu hili nilisome kidogo. Wizara hii ya Mawasiliano imo katika Idara ya Mawasiliano inasema kwamba.

> "Idara inajukumu la kusimamia maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano na kuratibu masuala ya taasisi za mawasiliano za Serikali ya Muungano zilizokuwepo Zanzibar, katika maendeleo ya Teknolojia, idara itakuwa na jukumu la kuratibu na kusimamia uwekaji wa miundombinu ya mawasiliano ikiwa ni pamoja na mkonga wa kitaifa na kudhibiti matumizi na utoaji wa huduma za teknolojia ya habari IT."

Mhe. Mwenyekiti, lakini hata katika hotuba ya Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais tunaambiwa kwenye Afisi ya Vitambulisho hata sijui inahusika vipi, kwamba wao wamejiingiza na wao pia wanajiingiza katika utekelezaji wa mradi wa *E-Government*. Kwa hivyo inaonekena Mheshimiwa, ndio maana nikasema katika mchango wangu jana kwamba hapa pana harufu mbaya. Sasa hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, nataka Waziri nikubaliane naye lakini kwenye kitu kimoja. Hili suala zima la ujenzi akubali hapa lihamishiwe katika wizara inayohusika ambayo ni Wizara ya Mawasiliano.

Pili akubaliane na mimi kwa sababu kasema mwenyewe kwamba yalipotiwa saini makubaliano haya ya mkopo ilikuwa halijajulikana hili suala la kwamba Zanzibar itaingizwa katika *phase II* ya mradi wa Muungano, sasa hivi katwambia inaingizwa. Kwa hivyo hatuna haja ya kutumia gharama za Zanzibar kwa kuwaingiza katika deni kubwa walipa kodi wa Zanzibar wakati kuna sehemu ya mradi huu utagharamiwa kupitia fedha ambazokuwa ni haki yetu kupitia Serikali ya Muungano kwa sababu suala hili lipo katika mambo ya Muungano.

Kwa hivyo nilikuwa naomba anambie mambo hayo mawili katika hoja hii moja kwamba Je, anakubali kuwa suala hilo tulipeleke Wizara ya Mawasiliano nimruhusu tuendelee na kifungu hiki. Pili ananiambie kwamba zile fedha ambazo zitakuwa tumezipata kutokana na *Phase II* ya mradi huu kutoka Serikali ya Muungano basi itakuwa *deducted* katika hizi bilioni 30 na badala yake zitakwenda kufanya shughuli nyengine katika maendeleo ya wananchi wa Zanzibar. Naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimwambie Mhe. Jussa hayo anayoyaeleza yote ni sahihi kabisa wala hakuna mushkeli katika hili. Lakini nataka nimwambie vile vile kwamba wakati wa uandaaji na utekelezaji wa suala hili kulikuwa kuna kamati ambayo ilihusisha watu wa mawasiliano na miundombinu. Lakini hili analolisema kwamba kuambiwa miundombinu waisamamie ujenzi hiyo ni jukumu lao wala halina matatizo kusimamia ujenzi, sisi ni waratibu na ndio maana liko pale kwa sababu ya kuratibu, na sisi tutawaandikia hasa miundombinu kwa sababu wao ni *technical now how* iko kwao wasimamie tutafanya hivyo halina matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili ambalo alilolizungumza Mhe. Jussa hapa pana utata kwa sababu ile *second design* bado haikuja Zanzibar na mimi sikuiona wala Waziri wa Miundombinu hanayo hivyo hatuwezi tukasema kwamba Zanzibar imo mle ndani. Mhe. Mwenyekiti, isipokuwa Waziri wa Mawasiliano wa Muungano kasema kwamba na Zanzibar itaingizwa katika *phase II*. Mhe. Mwenyekiti, lakini la msingi hapa hata kama ukiingizwa kwenye *phase II* huna *ownership* haya ni masuala ya kiuchumi haya tunataka tutoke huko kwamba wao wawe na ownership tunataka kumiliki wenyewe. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachosema kwamba suala hili tuachiwe sisi wenyewe badala ya kutumbukizwa kule.

Mhe. Mwenyekiti, majadiliano yatakuja kama kuna pesa ambazo zimeonekana katika *phase II* hizi ni kwa ajili ya Zanzibar tuna masuala mengine mengi yakufanya katika mambo hayo hayo. Mhe. Mwenyekiti, tutakaa na Wizara ya Fedha ya Muungano na tutashirikiana na tutahakikisha tunashirikiana nayo kabla hawajamaliza ile *frame work*, hilo tutalifanya.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri na kuhusu hili la pili alilolizungumza baada ya maelezo yake naomba nikubaliane nae kusubiri hayo maelezo kwa sababu kama kuna fungu letu tuendelee kulidai kwa sababu ni haki yetu, umiliki nakubali ubakie kwa Zanzibar, kama alivyosisitiza. Lakini kuhusu hilo la mwanzo nataka anihakikishie tena ili tuendelee kwa sababu hizi lugha zilizotumika kusimamia au kuratibu nataka nihakikishiwe kwamba ule ujenzi wenyewe kwa huu mgonge, hizi fedha sawa zitakuja kwa sababu wao ndio washika fedha. Lakini masuala yote ya ujenzi yataondoka kwenye Ofisi ya Vitambulisho yatatoka katika Wizara ya Fedha masuala ya ujenzi kwa ukamilifu wake yatakwenda katika Wizara ya Mawasiliano, na fungu hili litapelekwa Wizara ya Mawasilino ili likasimamie kazi hii tusibitishe linafanywa kitaalamu na sio mradi wa watu wachache wakataka kujinufaisha. Naomba kauli iwe thabiti ya Mhe. Waziri ili nimruhusu tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba hapa kidogo kuna lugha baina ya mimi na Mhe. Jussa na sijui kwa nini Kiswahili chetu kinatofautiana kwa sababu mimi ni wa Vikokotoni na yeye ni wa Mwembetanga. Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kuhusu ujenzi tutawaachia mawasiliano wasimamie.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru tuendelee.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii kidogo nipate ufafanuzi. Kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake ya ufasaha na takriban masuala tuliyouliza ametujibu ingawa kutokana na muda kama alivyosema kuna baadhi ya mengine hakuyatolea ufafanuzi, lakini tutapoendelea katika vifungu tutamuomba atusaidie ufafanuzi vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu inakuja nilipokuwa nikichangia nilijaribu kuzungumza mambo mengi na kuna baadhi ya mambo nilipoona kwamba kuna baadhi ya majibu kila siku yanatolewa hayaturidhishi nikataka Mhe. Waziri kama hajanitosheleza kwa jawabu na yeye itabidi uniruhusu ukubali kuunda Kamati ya Baraza ili tukajiridhishe. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ikiwa kila siku leo waziri huyu anatujibu hivi ndio pale tunapopata mashaka. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka ufafanuzi katika hili kama haujanitosheleza itabidi uniruhusu twende kwenye kamati kwa mujibu wa kanuni zetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hoja yangu ilikuwa ndani ya kitabu cha Mhe. Waziri nilisema ilikuwa ukurasa wa 2 kifungu cha 9 katika kusimamia mali za serikali. Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na utata mkubwa katika mali za serikali, na utata wetu unakuja zaidi katika viongozi wetu wanapojibu hasa masuala hapa yanapokuwa waziri huyu akija anajibu hivi na waziri mwengine anajibu hivi ndio pale yanatupa mashaka. Halafu ni kwamba mali zenyewe za serikali tunaziona zinayoyoma Zanzibar wenyewe ni ndogo.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka ufafanuzi kwani nilipokuwa nikichangia nilieleza namna ya maeneo yanavyotolewa wakati mwengine tuseme kiholela au wakati mwengine watu wanatumia nguvu kuyachukua haya maeneo bila ya taratibu mzuri. Mimi nilitaka ufafanuzi juu ya kiwanja cha Living Stone House na hapa ingawa samahani kidogo Mhe. Mwanasheria Mkuu aliwahi kutoa ufafanuzi alitoa hadithi ya Abaabeli, lakini Abaabeli wa zamani na wa leo ni tofauti. Abaabeli wa zamani akiona mwezi bado macho yake yanaona ule ule mwezi, lakini Abaabeli wa leo wakiona mwezi na nyota pia wanaona. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, yale ya zamani tunayakumbushia tulikuwa tunayatilia nguvu na hizi ndio taratibu zetu kwa sababu mheshimiwa na wewe ukubali na sisi tuunde kamati mpaka tukuridhishe na kukuridhisha kwetu tunaelezea hili hatulikubali, lakini tulikubaliana na wewe kwamba tuendelee. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi sisi tunaona nyota na mwezi.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaja na maeneo mengine na Mhe. Mwanasheria Mkuu yeye hakusema vile alitaka asaidiwe ufafanuzi kwa sababu yeye sio mwana siasa. Ndio maana nikamwambia ajibu ya kisheria ya siasa atuachie wenyewe. Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la kamati ambayo ulioiruhusu ya mawasiliano mimi nilitaka Kamati Teule lakini ukairuhusu Kamati ya Mawasiliano ikafanye kazi. Mimi ninavyojua kwa taratibu zetu Kamati ya Mawasiliano kuna maeneo ambayo haihusiani na wizara ile haiwezi kwenda kufanya uchunguzi. Mhe. Mwenyekiti, ndio maana Mhe. Mwanasheria Mkuu atuachie wenyewe tunapogusa gusa kule tukakazia kazia tunataka kuthibitisha kwamba hata ile kamati ambayo ingeundwa maeneo haya mengine isingefika. Kwa mfano, nilitaja kama eneo lilofukiwa unajua ukeshakuunda tume au kamati utaipa hadudi rejea haiwezi ikafanya kazi nje ya maeneo yale.

Mhe. Mwenyekiti, kwa busara za Mhe. Balozi na wewe bajeti hii leo itapita, Waheshimiwa Wajumbe kwa busara za Mhe. Balozi na wewe basi bajeti hii itapita. Lakini hapa nipe nikupe! Mhe. Mwenyekiti, tusishughulike sana atujibu kuhusu kiwanja cha Living Stone na yale maeneo kwa sababu nikija suala la Mtoni pale nilikuwa naona kamati ile haiwezi kwenda kufanya kazi, lakini pale pana uwekezaji ina maana tupate vibali vya *ZIPA*. Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikasema mheshimiwa tumpe muda akatafute vibali vyote vile tulivyoomba na mheshimiwa akitaba tubishane sana kuna maeneo mengine mengi tutakuja kuyataja hapa sio vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba busara itumike ili kwa kweli mheshimiwa kamati zako si unaziamini, mbona zitafanya kazi vizuri na tutakuletea ripoti ambayo haina wasi wasi. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hii hoja ya Mhe. Waziri aliyosema kuna baadhi ya maeneo yanakuwa sio ya wizara yake ndio lilokuwa halikuridhisha, kwa sababu kuna ufafanuzi umeshawahi kutolewa kwamba *ZRB* wamepewa kiwanja kile, taarifa tulizokuwa nazo mpaka sasa hivi ni kwamba kiwanja kile anacho mtu binafsi. Mhe. Mwenyekiti, kama ingelikuwa mawaziri wanakuwa na kauli moja wote sisi tungekuwa hatuna mashaka, lakini waziri huyu akisema hivi na waziri huyu akisema hivi ndio tunapata mashaka. Mhe. Mwenyekiti, naomba jawabu.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, nilieleza mwanzo kwamba mzigo mzito mpe mwanyamwezi, hili suala la viwanja nimesema kwamba halihusiani kabisa na ofisi yangu. Lakini kwa sababu niko ndani ya serikali nitasaidia kutoa ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kiwanja cha Living Stone kilikuwa kiko chini ya Wizara ya Kilimo, Ofisi yangu ya *TRA* wakati inatafuta eneo la kujenga Ofisi ya Makao Makuu wakaambiwa kwamba wawasiliane na Wizara ya Ujenzi ili aweze kupatiwa eneo hilo. Mhe. Mwenyekiti, tukawasiliana na wizara ya ujenzi, ujenzi wakawasiliana na kilimo eneo hilo mkaambiwa mnaweza kwenda kuliangalia kama litakufaeni chukueni kwa maandishi.

Mhe. Mwenyekiti, watu wangu wa ZRB walipokwenda kuliangalia lile eneo wakasema kwa kweli sisi halitutoshi kwa aina ya jengo tunalotaka kujenga. Mhe. Mwenyekiti, yule aliyetuandikia sisi tuchukue lile eneo alikuwa ni Wizara ya Ujenzi sio kilimo. Mhe. Mwenyekiti, *ZRB* wakaandika kwa maandishi wakalirejesha lile eneo majenzi. Kwa hivyo, kama kuna majenzi katoa kwa mtu binafsi hilo haliko kwenye mamlaka ya Wizara ya Fedha tena kwa sababu *ZRB* ameshalirejesha lile eneo. Kwa hivyo, mimi na barua zipo mimi siwezi nikamwambia Mhe. Mwakilishi kwamba tunafanya nini katika hili, kwa sababu Wizara ya Ardhi kwa mujibu wa sheria ya ardhi wana mamlaka ya ardhi, wana mamlaka ya maeneo. Mhe. Mwenyekiti, mimi Wizara ya Fedha sina mamlaka ya ardhi, mimi nilivyopewa nimelirudisha na barua zipo na wakanijibu kwamba tumeshalipokea sasa wao majenzi kama wamelitoa wakawapa watu wengine mimi sina cha kujibu katika hili Mhe. Spika.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, jawabu imetoka juzi tu kwa sababu aliyekuwa Waziri wa Majenzi yupo ndiye aliyetoa kauli hii naomba ninukuu. "Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ghala la Living Stone hili suala aliuliza Mhe. Mtando ni kwamba maghala yote wamepewa *ZRB* ndio wanaojenga pale. Kwa hivyo, kama unataka ufafanuzi zaidi tumsubiri Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kwa hivyo, ndio tulikuwa tunasubiri jawabu ya Mhe. Waziri wa Fedha, leo anaposema halihusiani na yeye na *document* anazo, mimi *document* nilizitaka tangu jana kwa nini asije nazo anipe. Mhe. Mwenyekiti, mambo ya kuambiwa kachukue *document* kwa Spika hatutaki.

Mhe. Mwenyekiti, naomba turudi katika kanuni ya 117 ili turudi kwenye Baraza tukubaliane Mhe. Mwenyekiti, utuulize kama wajumbe wataridhie basi tuachie tu mimi nitakuwa sina tatizo. Lakini katika hili kuna mambo mengi ndio maana tunataka tuisaidie serikali. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kuna baadhi ya maeneo mpaka sasa hivi kama yamechukuliwa kibabe, kuna maeneo yamechukuliwa kwa taratibu za kisheria na yaliyochukuliwa kibabe yarejeshwe serikalini. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi serikali inawahamisha watu katika maofisi kwa sababu haina maeneo, leo kwa kwa nini tunachukua maeneo tunawapa watu binafsi halafu watu wanapakatana pakatana katika ofisi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi jana napigiwa simu na watu wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya pale wanalalamika wanasema tumekaa chini ya miti hatuna ofisi, hivyo kwa nini maeneo tunayo tunawapa watu binafsi. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sitaki tuseme mengi kwa sababu nitalia. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba turudi kwenye Baraza kanuni ya 117 ili tutoe maamuzi.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Spika, mimi nataka niseme tu kwamba sheria ya ardhi haikatazi mtu binafsi kumilikishwa eneo kwa ajili ya maendeleo. Nadhani kwamba Waziri wa Ardhi baada ya kurejeshewa hili eneo pengine kuna mtu alikwenda kuomba kwa ajili ya maendeleo akaona kwa sababu halina mtu basi ampe. Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwamba haikatazi sheria ya ardhi na ndio maana nikatoa mfano hata sisi tunapoomba ardhi kwa kujenga tunapewa ardhi kwa kujenga, haikatazwi. Kwa hivyo, kama kuna kifungu ambacho kinasema kwamba sheria ya ardhi inakataza, lakini mimi sheria ya ardhi ninayo haikatazi kabisa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mimi nafikiri kwa kuwa Wizara ya Ardhi wenyewe wapo hebu watusaidie maelezo basi.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima zote Mhe. Hamza tumemsikia kilio chake na malalamiko yake, sasa kama serikali na kiongozi wetu yupo tunamuahidi Kamati ya Ujenzi na Mawasiliano hayo yote tutayafanyia kazi. Hivyo tunamuomba atuachie kama alivyoahidi kwamba bajeti itapita na tunamuomba tuipitishe tunachukua ahadi sote humu tutakwenda kuifanyia kazi na yeye tutamshirikisha kama Mwenyekiti wa Kamati nyengine ipasavyo kuja kutupa hayo mambo mengine ambayo hatuyajui ili kamati hiyo ifanye utafiti uzuri na tufanikishe mambo halafu tuyalete hapa. Tunamuomba sana Mhe. Hamza.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, suala hili kama nilivyosema kwamba ni suala MTAMBUKA tukisema kwamba tuipe Kamati ya Mawasiliano mheshimiwa hoja nilizozijenga katika kamati iliyopita, ni kwamba kamati hii itachukua si chini ya mwezi mzima kufanya hiyo kazi. Kwa nini mheshimiwa wajumbe wengine wapo wa Baraza la Wawakilishi hawana kazi yoyote tukaibebeshe majukumu kamati moja kubeba mzigo. Mhe. Mwenyekiti, yale niliyoyaomba katika Kamati ile ya Mawasiliano mwezi mzima hautoshi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kama ingelikuwa mwenyekiti ningelikuwa nishakuletea hadudi rejea za maeneo ya kwenda kukagua. Kwa nini wajumbe wengine wasipate nafasi hii, mimi nimejenga hoja ya kanuni nilikuwa naomba Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako turudi kwenye Baraza ili twende tukafanye maamuzi. Kwa sababu jawabu zitakazotolewa hapa kwani tumeshatolewa jawabu na mawaziri mbali mbali hatukuridhika. Kwa hivyo, hapa tutaendelea kupoteza muda na leo Ijumaa tunataka tukasali kama nilivyosema Mhe. Mwenyekiti, hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri itapita hii bila ya matatizo yoyote lakini sio ipite tu lakini na yale tunayoyataka sisi kwa niaba ya wananchi turuhusiwe.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, kama maelezo aliyotoa Waziri wa Nchi Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwamba ni kweli kiwanja hiki sasa amepewa mtu binafsi, lakini Mhe. Hamza alitaka kujua hasa aliyepewa ni kweli amepewa mtu binafsi na kwa kuwa mjumbe wako anataka iundwe kamati ya kufuatilia jambo hili. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba serikali haina tatizo ya kuunda kamati.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, mimi ndio ninavyompenda Balozi Seif Iddi Makamo wa Pili wa Rais. Mhe. Mwenyekiti, katika michango yangu kuna maeneo mengi sio hili tu kwa hiyo nilikuwa naomba mheshimiwa katika hiyo kamati utakayoipa hiyo kazi basi uangalie *hansard* yangu katika maeneo yale ambayo nimeyagusa. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na namshukuru sana Makamo wa Pili wa Rais kwa busara zake, naomba tuendelee.

**Mhe. Mwenyekiti:**Ruhusa imeshatolewa isipokuwa nataka kutoa maelezo kidogo tu, ni kweli nakumbuka hata kwenye Wizara ya Habari kulikuwa kuna habari ya mikataba na pale tuliahidi kwamba kutakuwa na wajumbe wa kamati wafuatilie mikataba ile. Kwa hivyo, sisi kama uongozi huku tulisita kidogo kwa sababu kuja kuunda kamati nne au tano zote teule kidogo ni jambo ambalo itakuwa sio muafaka vyema, tunapaswa wakati huo huo tuzingatie matumizi ya fedha. Kwa hivyo, hili jengine na lile la mwanzo tutayakusanya mambo haya ili kamati hiyo teule sasa itakayoteuliwa iweze kupewa maeneo hayo ya kufanyia kazi. (*Makofi*).

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0401 | Idara ya Mipango na Sera na Utafiti | 107,796,000 |
| Kifungu 0701 | Idara ya Muhasibu Mkuu wa Serikali | |

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimsifu sana Mhe. Waziri na yeye ameweka historia katika Baraza hili kuwa mkweli na muwazi, hilo namshukuru sana. Lakini katika kujibu yake suala la *Rest House* Micheweni alisema kuwa ameshalipa, ningemuomba tu mheshimiwa anifahamishe alilipa mwaka gani kipindi cha kwanza na kipindi cha pili mwaka gani.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, labda niseme tu Mhe. Mshimba hakunisikia vizuri Rest House ya Micheweni sikuigusa niliyoizungumza ni Rest House ya Wizara ya Fedha na sikuigusa Rest House ya Micheweni kwa sababu hii inashughulikiwa na na Mkoa wa Kaskazini Pemba wenyewe.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, ni kweli labda nilikuwa sijasikia masikio yangu yameziba, lakini nilikusudia kuwa ile ni moja katika fungu ambalo lina sababu ya yeye kuwa anatoa fedha katika Mikoa na katika Wizara nyengine. Kwa hivyo, niliona labda na yeye anahusika na suala hili ndio maana nikasema kuwa Mkoa haujengeki kama si yeye kupeleka fedha. Kwa hivyo, kama hili anaweza akanisaidia namuomba Mhe. Waziri anisaidie kwa huyu mtu mpaka leo hajalipwa pesa zake kwa upole kabisa.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Mwenyekiti, kama tutakumbuka sote hili suala Mhe. Subeit alililiuliza na tukamtolea ahadi kwamba mwaka huu wa fedha Rest House ile itamalizwa, kulikuwa na migogoro mingi ya fedha na yule mjenzi alikuwa anashughulikia Rest House ile pesa alizolipwa kwa kweli zilikuwa nyingi mno bahati mbaya alifariki. Mhe. Mwenyekiti, alifariki na ndio mambo mengi kafa nayo bahati mbaya kwa hiyo serikali imechukua jukumu kwamba itaimaliza yenyewe.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, unajua sisi ndio haya mambo ambayo yanatuchanganya ukija waziri huyu anajibu hivi, akija huyu anajibu hivi. Lakini sasa hapa kuna barua kuna hii Alhaal *Construction Company* ambayo hiyo ndio muhusika mkuu haisemi aliyekufa. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, *Rest House* ya Micheweni ndiye aliyejenga huyu na akafika Mahakamani, na Mahakamani wakakubaliana kuwa wafanye mambo ya nje na wakakubaliana. Mhe. Mwenyekiti, ananiambia kuwa watalipa na yeye hayupo tena katika Wizara ile ya Fedha naomba anihakikishie lini utaanza kumlipa huyu.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Mwenyekiti, anayosema Mhe. Mshimba ni kweli yule bwana alikuja tusiende Mahakamani, lakini sisi hatukumkubali kwa sababu tumeona kwamba anatudanganya. Kwa sababu yeye hajui hasa ule ujenzi ulikwenda vipi, narudia tena kwamba tulikwenda na mjenzi vizuri na akalipwa karibu kumaliza pesa zake, bahati mbaya sana Mwenyezi Mungu amechukua roho yake. Kwa hivyo, hao wametokezea hawajui mwanzo wala mwisho kama wanataka kuturudisha tena kwenye ujenzi wote tukaa tukaoneshana vigezo vya pesa, tumetumia kiasi gani, anadai kiasi gani, utakuta kilichobaki ni kidogo mno. Kwa hivyo, yeye hakukubali ndio akenda Mahakamani, sasa hivi anasema turudi tena serikali haikukubali.

Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kwamba sisi tunakubali arudi lakini ni kwamba pesa nyingi sana tumeshampa. Mimi naomba sana kidogo inaelekea Mhe. Mshimba kidogo hii kesi ndefu sana kuipata ufahamu ningemuomba mimi tutashirikiana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo tuje tumfahamishe kama anataka zaidi kumuongoza huyo anayedai basi tumuongoze. Lakini naona kidogo maelezo yapo mengi na magumu nataka tufahamu hivyo kwa ufupi tu Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mmoja katika mtiifu sana, na niko tayari kukaa nao hawa lakini ningemuomba kidogo tu mheshimiwa nimpe reference ya barua ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo naomba kidogo kwamba huyu Mkuu wa Mkoa wa Kusini aliomba pesa hizo angalau apewe milioni 60. Kwa hivyo, hii sijui ilikuwaje na ikaelezwa kuwa habari ya vifungu hivyo kwa hiyo ningemuomba Mhe. Waziri akishanijibu hili basi tuendelee kuwa hii barua iliandikwa kwa makosa au vipi au ndio hizi milioni 60 zenyewe ndio katika hiyo kasma ndogo iliyobakia. Mhe. Mwenyekiti, kama ni kasma ndogo iliyobakia kwa hizi 60 milioni basi naomba apewe, naomba jibu halafu tuendelee.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini yeye ndiye dhamana kweli ile *Rest House* iko kwenye Mkoa wake, na bahati nzuri yeye ndiye aliyemtafuta huyo *original* mjenzi sasa kutuomba sasa hivi tumuongezee pesa nyengine mbali ya zile zilizotoka serikali haikukubali. Hivyo wizara ilimuagiza uje tukae pande zote, uje wewe na sisi tukae pamoja ili tubadilishane *notice* ili tuone kiwango gani cha fedha ambacho kililipwa na kiwango gani cha fedha kinachohitajika kuimaliza kazi na serikali itaimalizia kazi. Klwa hivyo, serikali haikukubali kumpa pesa hizo kwa sababu alikuwa hana takwimu za kutosha.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mimi nafikiri tusi-*rule out* kuhusu kutoa fedha au la, isipokuwa Mhe. Mshimba umeombwa na Mhe. Waziri kwamba haya masuala muyaangalie pamoja kwa mashirikiano ya Mhe. Waziri. Kwa hivyo, kama itakuwa bado hakuna muafaka baada ya mashirikiano na waziri pamoja na Waziri wa Fedha ichukue hiyo ni sehemu ya kazi ya kamati kulifuatilia hilo.

| | | |
|---|---|---|
| Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | | 1,677,593,000/- |
| Kifungu 0801 | Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar es Salaam | 190,571,000/- |
| Kifungu 0901 | Idara ya Fedha za Nje | 109,586,000/- |
| Kifungu 1001 | Idara ya Mipango ya Maendeleo na Watendakazi | 136,243,000/- |
| Kifungu 1101 | Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Sekta na Kupunguza Umasikini | 262,970,000/- |
| Kifungu 1301 | | |

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi kidogo nipate ufafanuzi juu ya suala langu hili. Nilipokuwa nachangia nilizungumzia juu ya suala la jengo la Mambo Msiige, nilimtaka Mhe. Waziri anipe maelezo ya kina juu ya jengo lile namna gani lilivyotoka na utaratibu mzima. Lakini katika majibu yake Mhe. Waziri hapa amejibu kwa mkato tu, jengo le Mambo Msiige bado ni la serikali hatuuzi na ni mali ya serikali. Kwa hivyo, nataka kujua kwamba limekodishwa kwa utaratibu upi, kiasi gani, gharama zilizotumika kuwahamisha wale wafanyakazi waliokuwa wanatumia jengo lile kwenda maeneo mengine. Naomba ufafanuzi katika hilo Mhe. Mwenyekiti na utaratibu mzima ambao ulitumika kuliondosha.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe.. Mwenyekiti, kama tutakumbuka katika Baraza hili suala hili nimeletewa maswali mawili juu ya jengo hili na nikajibu kwa kirefu. Lakini hata hivyo, naomba niongezee tena kumsaidia Mhe. Mjumbe maswali yake kama ifuatavyo.

Kwanza jengo hili tuna nia ya kulikodisha, nasema tuna nia kwa sababu hatujasaini mkataba wa kukodisha. Nilizungumza mwanzo kwamba mkataba uliopo ni ukodishwaji wa ardhi ya eneo lile, hekta 0.42 kwa dola elfu kumi kwa mwaka ardhi, sio jengo. Jengo nimesema tutakuja baada ya kufanyiwa ukarabati tuone uzuri wa jengo letu ndio tukae tunaamua tunalikodisha kiasi gani.

Lakini nilijibu, kwamba wafanyakazi waliokuwepo katika maeneo yale wengine wamehamia majengo yao kama Idara ya Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti wamehamia kwenye jengo lake, Shirika la Meli wamehamia kwenye majengo yao, nikasema kwamba Mrajis pamoja na Wakfu *PBZ* tumetumia jumla ya shilingi 170,000,000/- kukarabati jengo la *PBZ* na tumetumia shilingi 8 milioni kuwahamisha kuwapeleka katika jengo lile la *PBZ.*

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri mimi nahisi kuna utata kidogo. Mhe. Waziri anatwambia kwamba amekodisha dola elfu kumi lile eneo la kiwanja, jengo bado. Kipi kiliharakisha kwamba watu wale wahamishwe wafanyakazi na document zetu ambazo za miaka hiyo tunalalamika katika hili, wahamishwe kupelekwa katika eneo jengine wakati hamjafanya umkataba na huyo mnayetaka kumkodisha au unaefikiria kumkodisha. Hii mimi napata utata kidogo Mhe. Mwenyekiti. Kwa sababu jambo halijawa tayari wewe umeshahamisha watu unataka mtu yuje aje atengeneze ndio muweke mkataba, mimi kitu hiki nakiona kiko kinyumenyume kabisa. Naomba ufafanuzi zaidi katika hili.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mawili hapa namuomba Mhe. Mtando kwanza akubaliane na mimi. Kwana jengo ni bovu, katika hatua niliyozungumza ni kwamba yale majengo ni mabovu hili ni moja na akitaka sasa hivi Mhe. Mtando tukimaliza kikao mimi na yeye tutakwenda tukaliangalie hali ya jengo. Ndio maana tukasema kwamba nafasi tuliyoipata ya kuweza kuwahamisha hawa kabla jengo halijawaangukia ni nzuri.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, huwezi ukafanya maamuzi ya kutaka kuwakodisha jengo watu kama ndani mna watu, lazima kwanza muwahamishe wale ili mfikie muwafaka wa kusema sasa tunaaza kukodisha. Sasa mimi nataka nimwambie Mhe. Mtando kwamba lile jengo hali yake ni mbovu.

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, mimi sikubaliani na mawazo ya Mhe. Waziri. Jengo lile wafanyakazi walikaa pale wanafanya shughuli zao kuna taarifa yoyote rasmi ya maandishi ambayo inasema jengo lile ni bovu na watu wahame?

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, katika utafiti wa Sera ya Taifa ya Nyumba jengo lile limefanyiwa utafiti pamoja na majengo mengine limebainika jengo lile ni bovu. Wenzetu wa Benki ya Dunia walipotaka kutusaidia katika ku-*computerize* zile *document* zilizomo mle ndani wakatwambia hiyo *computerization* kwa jengo hili hatuwezi tukakufanyieni, lazima mjenge jengo jipya. Hayo hayatoshi kuweza kuhama?

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, naona waziri anakimbia kwenye hoja. Hoja yangu ya msingi kuhamisha watu juu ya ukodishwaji wake kama ambavyo amesema halijakodishwa. Sasa kuna kipi cha kuwahamisha. Hiyo ripoti ni ya mwaka gani. Mimi nafikiri Mhe. Mwenyekiti, tusitupe muda mwingi sana tuingize katika ile Kamati Teule utakayoiunda liwemo na hili katika kuchunguzwa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mzazi na mimi nimezaliwa, naogopa sana jengo lile hali yake ilivyo. Tulipokwenda kulikagua na Makamo wa Pili wa Rais mimi niliogopa kwa maana kwamba linaweza likadondoka na Makamo tukanae ndani, shahidi Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Fursa tuliyoipata wenzetu hawa wametusaidia dola milioni moja na nusu, wamesema hizi tunakupeni kama msaada wetu kuwajengea jengo jipya. Sasa jamani Mhe. Mwenyekiti, fursa kama hizo tunaziacha. Kuna *study* zimeshafanywa, tathmini, majengo mabovu yote ya serikali tunazo taarifa zake ikiwemo pamoja na lile na uharaka wa kuwahamisha wale watu ni kuwanusuru watu wetu.

Mimi nataka nimwambie Mhe. Mtando mimi kwenye jengo lile nilijisikia vibaya sana hali yake ni mbaya, tumewahamisha *on the right time* tungekaa mpaka likaanguka ndio tukawahamisha watu wakati ripoti za tathmini zimeshatoka tungekuja kulaumiwa serikali mmechukua hatua gani muda wote, zimeshatoka na ripoti hizo Mhe. Mwenyekiti, zimethibitishwa na Baraza lako hili hili, hiyo sera imepitishwa na Baraza lako hili, lingeanguka lile jengo ndugu zetu na watoto wetu wamo ndani Wallahi Mhe. Mwenyekiti, tungekuja kulaumiwa sisi serikali tumefanya nini. Tumefanya hatua nzuri namuomba Mhe. Mtando akubaliane na hili juhudi tunayochukua serikali wakati mwengine jamani tuipongezeni. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** nadhani hapa hapana kazi kubwa, jengo maelezo kwamba ni bovu. Mhe. Mtando yeye ana wasiwasi basi acha hiyo kamati ikajiridhishe.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa jinsi anavyojibu hoja kwa ufasaha na niungane kabisa na mchango wa Mhe. Mwanasheria Mkuu wa jana ambao aliwakanya Wawakilishi tusije tukawa kama Mahababegi. Lakini naomba niongezee tu kwamba mbali ya kuwa mahababeli tukawa kama vile shehe aliyekataa nyama ya kuku ya wizi akanywa mchuzi.

Mhe. Mwenyekiti, nilipohoji hapa nilisema kwamba mwaka juzi baada ya tatizo la umeme Zanzibar kutokea, ndugu zetu wa *UNICEF* walitusaidia majenereta zaidi ya 12. naomba kujua tu, yako wapi hivi sasa hapa Zanzibar.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuombe radhi ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija katika masuala ambayo sikuweza kuyajibu moja ni la kwake. Majenereta tuliyosaidiwa yalikuwa ni 12 na tumesaidiwa na *UNICEF*, alitaka kujua kwamba majenereta hayo yako wapi. Nataka nimwambie kwamba majenereta hayo yamefungwa katika katika vituo 12 vya maji na sasa yapo hapo naomba nimtajie.

Kiashangwe liko moja, Donge 1, Kitogani 1, Machui 1, Bambi 1, Chaani 1, Unguja Ukuu 1, Jendele 1, Kianga 1, Kinyasini 1, Kandwi 1 na Makunduchi liko moja.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, kaka yangu amenijibu kwamba majenereta yote yapo na ametaja maeneo tofauti. Kwanza nikushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwamba wawakilishi wanapopewa uspika wana haki ya kupewa uspika. Kwa sababu kama kila mtu atahoji kuunda kamati wajumbe wote watapewa kamati. Kwa hivyo, busara zako kwamba kila penye shaka kamati yako itafute ni sahihi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri amenambia majenereta 12 yako maeneo hayo, Wazanzibari wanasema kwamba wanayajua mengine yalipo. Sasa kuna haja ya Mhe. Waziri nikuombe Mhe. Mwenyekiti, kwamba ile kamati ambayo itachaguliwa kwa busara zako baadae itafute vyema hadudi rejea. Kwa sababu jarida kama hili nililonalo mimi jana nimelitafuta pahala nimeliona na sio katika maeneo ambayo ameyataja. Kwa hivyo, nikuombe Mhe. Mwenyekiti, kwa hoja hii ili nikupe nafasi uendelee mbele niwaombe wale wenye busara ya kamati baadae wakichaguliwa wazingatie hizi hansard watafute ukweli ulivyo juu ya mali za serikali. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, maelezo mazuri yaliyotolewa na Mhe. Waziri, lakini Mhe. Mwakilishi ametuonesha kwamba kuna wizi umefanyika kwa mujibu wa maelezo yake wa majenereta hayo. Kwa hivyo, namuomba atukubalie serikali ifanye uchunguzi kwa kupitia vyombo vyake ili iweze kujua kama yapo yaliyoibiwa na hatua za kisheria zichukuliwe.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, bahati mbaya sikumsikia vyema kwa hivyo, naomba ile hoja anisaidie.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, ningependa nirudie maelezo yangu. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kuhusu masuala ya jenereta na kwa maelezo ya Mhe. Hija inaonekana kuna wizi umetokea. Namuomba atukubalie serikali ifanye uchunguzi kupitia vyombo vyake ili kuona kama kuna wizi hatua za kisheria zichukuliwe.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza kwenye maelezo yangu haya sijasema kama kuna wizi, nimesema wananchi wana wasiwasi wa ugawaji wa majenereta yalipo na nimesema kwamba kuna wasiwasi vile vile kwamba kuna moja liko Kilimani. Sasa wasi wasi wa kuwa pahala sijasema kuwa wizi lakini kama anataka anisaidie kwamba hapo lilipo pana wasi wasi atanisaidia Mhe. Waziri, lakini si hisia zangu kwamba kuna wizi. Nitamsaidia wasi wasi wa wananchi lilipo hili jenereta akalione kama ndilo atanambia.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo yake kuwa tushirikiane naye tupate maelezo ya ziada tuchukue hatua zinazofaa.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na nimefurahika sana na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini katika hoja hii niliichangia mimi na sikusema kuwa hawafanyi kazi kuwa wana nini aa, nilisema hapa nyenzo hawapewi, zile nyezo hasa za kufanyia kazi wanafanya kazi katika mazingira magumu na ndio maana nikasema nitakuwa mkali katika kifungu hili cha Uhakikimali. Sasa namuomba Mhe. Waziri aniridhishe kuwa hizo nyezo atawapa lini na maposho yao hawapewi kikawaida.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Makame Mshimba aligusia habari ya nyezo. Nataka nimuahidi kwamba nitaiangalia hii Idara ili niweze kujua mahitaji yao halafu tutawasaidia ili waweze kutekeleza majukumu yao vizuri zaidi.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, mimi namuamini sana Mhe. Waziri na hasa akinialika na mimi niende ofisini kwake. Tuendelee.

Kifungu 1301 Idara ya Uhakikimali na Mahitaji ya Umma 197,604,000/-
Kifungu 1901 Idara ya utawala na Huduma

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, pale awali nilisema nilikuwa na hoja mbili, naona nitumie idara hii yenye mshahara wa Mhe. Waziri anisaidie maelezo kidogo. Katika mchango wangu wa jana Mhe. Mwenyekiti, niligusia suala la *BoT* na nilizungumzia mambo mawili, *BoT* na *TRA*. Nilizungumza suala la uwezo wake wa kumiliki uchumi ambao umeshatolewa ufafanuzi nashukuru sana, lakini pia nilizungumzia suala zima la muundo wa vyombo hivi na uwakilishi wa Zanzibar.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Mhe. Waziri na akatoa wito hapa kwa Wazanzibari kuitumia fursa itakayokuja ya kudai. Lakini nilikuwa nasema kwamba kwa kipindi hiki ambacho tunasubiri mchakato wa katiba, hivi waziri hana njia zozote za kufanya ili akatuhakikishia kuwa huu muundo wa *BoT* ambao umo humu katika watendaji 80 waliyoorodheshwa huku mwisho, mpaka katika Tawi la Zanzibar wote watendaji wanatoka Bara na Wazanzibari ni wawili tu. Sasa nataka anisaidie kwa kipingi hiki hakuna njia ya kutusimamia akiwa yeye kama waziri wetu tukahakikisha kuwa taasisi hii muundo wake una-*reflect* mpaka hapo suala litakapokuja kumalizwa katika mjadala wa katiba? Namuomba Mhe. Waziri anisaidie.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nataka nikubaliane na Mhe. Jussa, kwamba kama yeye linavyomuuma kuona Wazanzibari ni wachache katika taasisi za Muungano na mimi linaniuma hivyo hivyo. Lakini nadhani Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jussa atakubaliana na mimi kwamba katika maelezo yangu nilisema kuwa hivi sasa mawaziri wetu wawili hawa wa Utumishi Muungano na wa Utumishi wa Zanzibar wako katika vikao kujadiliana jinsi ya idadi ya Wazanzibari watakaoajiriwa katika taasisi za Muungano. Nadhani wako katika mazungumzo yanasogea sogea katika kufikia Muwafaka. Namuomba Mhe. Mwakilishi avute subira kidogo tukishakufanikisha mazungumzo haya mambo yetu yatakwenda vizuri.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, nakubali naomba tu, huo muwafaka utaokuja kufikiwa au sijui yatakuwa maridhiano biana ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumisi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar na yule mwenzake wa upande wa pili basi hiyo ripoti tuletewe Barazani tujiridhishe na sisi vile vile kwamba kiasi gani haki na maslahi ya Zanzibar yanalindwa na kusimamiwa ipasavyo. Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kukubaliana na mawazo mengi ambayo tumeyatoa katika hatuba hii. Tofauti na wale wengine waliofikiria kwamba labda sisi tuna chuki na watu fulani.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia suala zima la *BoT* nilieleza kutokuridhika kwangu na huduma zinazotolewa na *BoT* kwa Zanzibar, wakati *BoT* ni chombo cha Muungano na mpaka hivi sasa serikali yenyewe inadai kwamba hisa za Zanzibar katika *BoT* ni asilimia 11.5, wakati mpaka sasa hivi utekelezaji wake wenzetu Bara wanavyotulazimisha tunapata gawio la asilimia 4.5 ambacho ni kinyume na sheria. Katika kuendeleza muendelezo huo Mhe. Mwenyekiti, nimeeleza hivi, kuna fedha zilitolewa wakati wa msukosuko wa uchumi duniani, fedha nyingi na ndio maana nikamwambia Mhe. Waziri mimi kwa masuala yangu itabidi labda nikupe muda utafute hayo maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, juzi Naibu Waziri wa Fedha wa Bara tena ni Mbunge wa Zanzibar Jimbo la Chumbuni, aliulizwa Bungeni pale je, kuna taasisi ngapi zilizopewa pesa za serikali na za binafsi, fedha za *BoT* kwa kujihami katika msukosuko wa uchumi duniani, akataja akasema ziko karibu 96. Wabunge wakamwambia zilete, akasema kwa mujibu wa kanuni siwezi kuleta. Mhe. Mwenyekiti au alikuwa Spika wa Bunge akamwambia kwa mujibu wa Kanuni za Bunge chochote Wabunge wanachokitaka ukilete. Kwa hivyo, kapewa muda akaorodheshe yale makampuni au watu binafsi waliopewa pesa kwa aili ya kuimarisha makampuni yao.

Sasa hapa Mhe. Mwenyekiti, najua Mhe. Waziri kutokana na kuokoa muda na leo Ijumaa aliona mengine ayabakishe tunaweza tukayakumbusha kama hivi. Sasa hajatueleza je, kwa upande wa Zanzibar ambapo mimi mwenyewe binafsi nilimuomba *Governor* wa *BoT* katika kikao basi angalau aiwezeshe *ZSTC* katika ule msukosuko wa uchumi duniani kama Zanzibar na sisi tuna hisa. Ukiacha *ZSTC* je, kuna wafanyabiashara wengine au makampuni waliopata msamaha ule? Mhe. Mwenyekiti, nafikiri nikipata maelezo nitaendelea.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Hamza Hassan Juma ameuliza suala zuri na katika ile fursa ya muda tu nimefuatilia sana hakuna taasisi hata moja katika hizo aliyepata fedha za msukosuko.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Waziri pole sana. Mhe. Mwenyekiti, tunaposema Zanzibar tunaumizwa ndio mambo kama haya, taasisi 96 zimepewa pesa na pesa hizo Mheshimiwa sio mkopo, ruzuku basi hata Shirika letu la Serikali la *ZSTC*, *BoT* wameshindwa kutupa. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi nina wasi wasi na *account* ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuweko *BoT*. Hata haki zetu basi hizi tunazikosa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka maelezo *BoT* atatulipa pesa hizi lini, kwa sababu na sisi kama tuna *share* kama ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tuzipate. Kweli juzi Mhe. Mwanasheria Mkuu alisema Wabunge wetu wa Zanzibar wakadai kule, Waheshimiwa mmeshadai pesa hizi? Sasa sisi tunadai Mhe. Mwenyekiti, wabunge tuliopeleka watano (5) wale tumewawakilisha Bungeni sisi tunadai kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, tunataka kauli ya hili, inaonesha Mhe. Waziri hakuwasiliana vizuri na *Governor* wa *BoT* ndio maana nikasema hebu tumpe muda mpaka Jumatatu atuletee. Kwa sababu mimi naamini waziri angeliwasiliana na *Governor* wa *BoT* na kama angelisema *BoT* hapa tungeifukuza *account* yetu tukaweke SMZ pesa hizi zingeliletwa. Tunafufua *ZSTC* serikali mnatafuta pesa kumbe pesa ziko *BoT*, tunataka pesa zetu. Waanze *BoT* na wafanyabiashara wengine wazipate tena kwa hii hii 4.5, Kule makampuni 90 huku makampuni 35 tuendelee.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nmtoe wasiwasi Mhe. Hamza, nimewasiliana vizuri sana na *BoT* kuhusu suala hili kwa sababu hata na mimi lilinikereketa kidogo. Nikazungumza zaidi kuhusu habari ya *ZSTC*, lakini kwa sababu suala lililokuja jana ni kwamba mashirika mangapi yalifaidika na msaada huu ndio nikasema hakuna waliofaidika. *ZSTC* walifanyiwa tathmini wakaonekana kwamba *there not qualified*. Hayo ndio maelezo ambayo wametoa. Kwa hivyo, nimewasiliana vizuri sana na *BoT* la msingi ni kwamba inapotokea matatizo kama haya mimi nadhani tuwe *aggressive* zaidi pale linapotokea kuliko pale baadae.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nampongeza sana Mhe. Waziri, lakini kwa hili sikubaliani naye. Mhe. Mwenyekiti, fedha zimeshatoka makampuni 90, Zanzibar kama tuna hisa hili si suala la mjadala hili ni suala la agizo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Waambiwe *BoT* mtikisiko wa uchumi duniani na sisi ulitukuta, Shirika la *ZSTC* kusema halina vigezo kama lilikuwa halina vigezo ndio lilikuwa liwezeshe hayo ya Bara yana vigezo gani. Mimi nadhani tupewe kauli ya serikali, *Governor* wa *BoT* aidha tumwite hapa atueleze na sio tumwite tu, tupate gawio letu, makampuni tisini wataalamu wa hesabu fanyeni *calculation* asilimia 4.5 ya makampuni 90 ni ngapi, hii ni haki ya Zanzibar na lazima tupewe.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe muda unatoweka, leo siku ya Ijumaa na tusingependelea kuongeza muda kwa sababu ya Ijumaa na umuhimu wake. Hivyo turudi kwenye Baraza na kipindi hiki hadi jioni kitasaidia kuweza kutafuta maelezo muwafaka zaidi.

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe tuje jioni na hapa tulipofikia tumeshanote. Mhe. Waziri kwa hili na mengineyo jipange vizuri pamoja na serikali kwa ujumla ili tuje tumalizie jioni.

Kuna tangazo moja, Waheshimiwa Wajumbe Wawakilishi wanawake wanaombwa wabaki kidogo mara baada ya kuahirisha kikao hiki kuna maelezo watapewa. Kuna marekebisho kidogo, Waheshimiwa Wajumbe wanawake wa CCM wabaki kuna maelezo fulani wapewe. Baada ya hayo basi naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni, lakini tujitahidi tufike mapema ili tuhakikishe kwamba tuna *quorum* ya kupitisha vifungu.

*(Saa 6:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

## KAMATI YA MATUMIZI

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kurudi mapema ili tuendelee na kazi kwenye Kamati ya Matumizi. Hoja ya Mhe. Hamza Hassan Juma ilikuwa masuala yanayohusu mtikisiko wa uchumi ambapo upande wa Zanzibar hakuna shirika hata moja ambalo limepata ruzuku hiyo.

Sasa jambo hili limemshtua Mhe. Mjumbe nadhani pengine na Wajumbe wengine na akataka maelezo zaidi basi serikali inachukua hatua zipi juu ya jambo hilo.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako labda kidogo nitoe historia ili tuweze kufahamiana na kufahamu yaliyojiri wakati ule.

Mwaka 2007/2008 ulipotokea mtikisiko wa kiuchumi kuna baadhi ya makampuni yalieleza kwamba yaliathirika na mtikisiko huo na hasa walioathirika walikuwa ni hawa wa kati. Ni makampuni ambayo yananunua bidhaa halafu yanauza nchi za nje.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliiagiza Benki Kuu ya Tanzania *(BoT)* kuangalia, kupitia mabenki ya biashara, makampuni ambayo yamekopa na yameathirika kutokana na mtikisiko wa uchumi. Kwa hivyo, makampuni yale yakapeleka vielelezo vyao, kimsingi kulikuwa kuna mambo mawili. La kwanza ionekane katika hesabu zako za benki kwamba umenunua mazao kwa bei fulani na wewe umelazimika kuyauza kwa bei fulani ambayo ni kidogo ya ile. Fedha ambazo ulizonunulia mazao yale umezikopa kupitia benki na benki zenyewe ndio zikawasilisha hizo taratibu kwa mashirika yao.

Sasa ilipokaa Zanzibar mwaka huo mimi sikuwepo wapo wenzangu ambao walikuwa Mawaziri humu ndani, walipokaa Zanzibar wakaona kwamba *ZSTC* ipelekwe, *PBZ* akaipeleka *ZSTC BoT* kwa sababu ndio *banker* wake. Ikaangaliwa *ZSTC* ikaonekana licha ya kwamba bei ya karafuu ilishuka lakini *ZSTC* haikula hasara. Mhe. Mwenyekiti, taarifa kamili tunazo.

Kwa maana hiyo, *BoT* akasema kwamba *ZSTC* wewe huja-*qualify* kupewa msaada huu na zile pesa sio za *BoT*. Mimi nilikuwa Naibu Waziri Muungano zile pesa zimetolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na masuala ya kiuchumi haya si masuala ya Muungano. Kwa hivyo, *ZSTC* haija-*qualify* kupewa fedha zile, *PBZ* na *BoT* wakaridhika ikarudi.

Kwa hivyo, katika hili kwa kuwa ni suala lililotokea mwaka 2007/2008, mwaka 2009/2010 halikushughulikiwa na majibu sahihi ndio hayo. Mimi nadhani serikali itakuwa haina tena majibu katika suala hili kwa sababu suala limeshafungwa na *ZSTC* yetu haija-*qualify*. Ingekuwa ime-*qualify* basi mimi nina uhakika *ZSTC* wangepatiwa msaada ule.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kuweza kunivumilia nikapata maelezo ya kina kutoka kwa Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, mimi naendelea sana kumshukuru Mhe. Waziri kwa kila zile hoja ambazo tunazohisi zina uzito na zina utata kuweza kututolea ufafanuzi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania wakati wa mtikisiko wa uchumi duniani alikuja Zanzibar na akatutolea ufafanuzi wa namna mtikisiko wa uchumi duniani na zile taasisi zitakazoathirika na mtikisiko ule wa uchumi duniani. Yeye alivyotwambia kama *BoT* sio Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, kama ingelikuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano angelikuja Waziri wa Jamhuri ya Muungano anayeshughulikia Masuala ya Fedha. Lakini alikuja Gavana wa *BoT* na pale ndio maana tukajaribu kumuulizia katika hizi taasisi ambazo mnahisi zinaweza zikaathirika je, *ZSTC* ambalo ni shirika la Serikali ambalo sisi mtikisiko wetu wa kiuchumi ukiacha huu uliotokezea duniani, lakini mtikisiko wa kiuchumi tuliokuwa nao ni wa muda mrefu mpaka katika mambo yetu ya Muungano tutaisaidia vipi. Alisema tutajaribu kuangalia na kuweza kusaidia.

Lakini vile vile haya makampuni kwa sababu mimi ninayo *bullet* hapa ya *Bank of Tanzania Annual Report* ya mwaka 2008/2009. Mhe. Mwenyekiti, ukifungua hii ukurasa wa 38 naomba kidogo niisome *paragraph* ambayo imeletwa na *BoT* yenyewe. *"The Overall Economic Performance. The Zanzibar real GDP growth decline to 5.4 percent from 6.3 percent registered in 2007.*

*Chapter 6 (21)* inasema:

*The slower growth rate was associated global economic slow down which adversely effected the service activity notable the tourism related sub-activities growth of service activities."* Huko mbele siendelei.

Mhe. Mwenyekiti, kwa tafsiri ya Kiingereza changu Gavana wa *BoT* hapo ametuletea hili. Mhe. Mwenyekiti, wanapotuletea *BoT* matabu haya watuandikie Kiswahili, mmenisikia nilivyosoma Kiingereza hicho lakini mmekifahamu.

Kwa hivyo, ina maana hapa wenyewe *BoT* wameeleza mpaka hapa katika sekta ya utalii imeathirika na ndio maana uchumi wa Zanzibar umeshuka kutoka asilimia 6.3 mpaka asilimia 5.4. Sasa Mhe. Mwenyekiti, tunaposema kwamba hili suala ni la Serikali ya Muungano lakini aliyekuja kutoa maelezo Gavana wa *BoT* na kwa sababu *BoT* ndio anaye-*regulate* uchumi wa nchi zetu hizi mbili.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikawa najaribu kuwa na wasi wasi. Hebu Mhe. Waziri ajaribu kunieleza kwa sababu pengine hili tabu linasema vyengine. Tunawaomba hawa *BoT* watuletee haya matabu kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu Gavana wa *BoT* ni Mtanzania, Bodi yake ni ya Tanzania, sasa hebu atueleze kwamba taarifa hii inayoelezea uchumi wa Zanzibar umeathirika kwa kiasi fulani na tukakosa gawio la *BoT*.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nilitaka vile vile *atleast* tupatiwe japo *breakdown* yale makampuni ambayo yalipatiwa zile fedha kutoka kule Bara. Kwa sababu kuna Taasisi za Serikali na Makampuni Binafsi au Vyama vya Ushirika tupate maelezo. Mhe. Mwenyekiti, hatuna ukaidi lakini tunataka tufahamishwe ili na wananchi waweze kufahamu.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeifahamu sana *concern* ya Mhe. Hamza Hassan Juma. Lakini nataka nimthibitishie kwamba mimi nilikuwa Naibu Waziri Wizara ya Fedha na Uchumi kwa upande wa Tanzania. Aliyeiteua *BoT* kusimamia masuala haya ni Mhe. Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Waliambiwa nyinyi simamieni mfanye uchambuzi na nyinyi myatazame mabenki gani yaliyotoa hiyo mikopo na haya makampuni myafanyie uchunguzi nyinyi.

Ndio kwa maana wale *BoT* ikawa wao wanalifahamu lile suala vya kutosha. Hata mimi mwenyewe nilikuwa kwenye kikao cha *Cabinet* alipoitwa Gavana kuja kuwaelimisha Mawaziri wa Muungano nilikuwemo vile vile. Kwa hivyo, pale tulimuita Gavana kufanya zoezi hilo.

Lakini concern ya Mhe. Hamza Hassan Juma mimi nakubaliana nae kabisa. Uchumi wetu uliathirika kwa sababu gani. Kwa sababu watalii wengi wanaokuja kwetu Zanzibar asilimia 84 ni wazungu wao wameathirika zaidi. Kwa hivyo, walipoathirika wazungu wakaona sasa hivi ile starehe ya kwenda kutalii tuache ndio kwa maana akawa anasoma Mhe. Hamza pale kwamba sekta ya utalii ndio iliyoathirika zaidi.

Kwa sababu sisi Zanzibar uchumi wetu ni *services oriented* tumeathirika kwa hapo. Lakini kwa sababu sisi tulioathirika kiujumla uchumi wa serikali na yale makampuni ya kitalii hayakuathirika kwamba yalikwenda kukopa yakauza bei nafuu, wale hawakupata wale watalii ndio kuathirika kwao. Kwa hivyo, wao hawakuwa na *loss* ndio tafsiri iliyokuja.

Kwa maana hiyo, sisi Zanzibar kiuchumi tumeathirika lakini kikampuni moja moja kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma pale hawajaathirika, maana yake hakwenda mtu au kampuni iliyoripoti kwamba mimi nimekula hasara kwa sababu bodi ilikwepa halafu nikauza kwa bei pungufu, hapa ndio tafsiri yake. Kwa yale makampuni ambayo yalikopa lakini kwa sababu haikufanya faida kubwa Serikali iliwaomba *BoT* wa-*reschedule* ile *repayment period* na ndio kwa maana wakapewa. Badala ya kulipia miaka miwili wale waliopewa mkopo kulipa miaka miwili wakaambiwa sasa mnaweza mkalipa miaka minne au mkalipa baada ya miaka mitatu ndio muanze kulipwa miaka miwili.

Kwa hivyo, kwa mtazamo huo mimi nakubaliana na concern ya Mhe. Hamza Hassan Juma ndio nikasema kwamba hapa sisi kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hatuna cha kusema isipokuwa mimi kama Waziri ninayesimamia Masuala ya Fedha nasema masuala haya yatakapotokea sisi tu-*react first* tusisubiri mpaka kukawa kuna *reactions* zinatoka nje mpaka *reactions* zimeshawiva ndio tunakuja. Mimi ninaamini tungehamasisha makampuni yetu ya ndani kwa wakati ule wangetufahamu na wangejitokeza waliokula hasara. Lakini kwa wakati ule hatujahamasisha hayajajitokeza iliyopelekwa ni *ZSTC* na *ZSTC* imeonekana kwamba hawakula hasara isipokuwa karafuu bei waliyokuwa wanategemea hawakuipata.

**Mhe. Spika:** Mhe. Hamza Hassan Juma maelezo ndio hayo yako wazi, taratibu zinafahamika, uwe umekopa na katika kufanya biashara zako umepata hasara. Sasa *ZSTC* haikukopa wala haikupata hasara. Hayo ndio maelezo na *condition* zake ndio hizo za kuweza ku-*qualify* katika kupata ruzuku ile ya *BoT* kufuatana na mtikisiko huo wa uchumi. Mimi nafikiri maelezo yanatosheleza na nadhani serikali iwe imepata changamoto juu ya jambo hili kwamba yatakapotokea mambo haya basi wafanyabiashara wetu waelewe. Si kutwa kuna wengine wamekopa lakini walikuwa hawana habari, kwa hiyo sasa ni changamoto ya serikali ili masuala haya yakitokezea basi haraka sana taarifa kwa wafanyabiashara wetu, kwa mashirika yetu iwe inafika. Nadhani tuendelee.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, niendelee kumshukuru Mhe. Waziri kwa jinsi alivyotoa ufafanuzi wa hoja zetu kwa niaba ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia hotuba hii eneo hili nilizungumzia suala zima la hisa ya Zanzibar kwenye Benki Kuu. Nashukuru Mhe. Waziri alinijibu vizuri kwamba wakati huo Benki Kuu inaanzishwa Zanzibar ilikuwa na *pound* 84,000, kwa maana ya asilimia 11.05 ya hisa ya Benki Kuu.

Sasa nilipoangalia gawio la mapato hayo ya mwaka jana Zanzibar tulipata milioni 600, mara hii nashukuru tumepata milioni 800 kwa utaratibu ule wa asilimia 4.5. Lakini hoja yangu ya kwanza ni kwamba hata hiyo asilimia 4.5 imeanza kutolewa mwaka 1994 wakati Benki Kuu ilianza mwaka 1966. Je, mapato yetu haya 1966 mpaka 1994 haya ya kati katil yako wapi.

Lakini nimnukuu Profesa Issa Shivji ambaye aliinukuu SMZ mwaka 1987 kwamba wakati huo SMZ ya 1987 ilidai riba ya hisa kutoka *BoT* ya *pound* 1,600 sawa sawa na 1.6 bilioni wakati huo. Sasa mwaka 1987 mpaka hii leo ni *trillions*. Mhe. Mwenyekiti, naomba kujua Serikali ya Zanzibar tumefikia wapi.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo unisaidie kwenye kanuni. Ninavyofahamu mimi ni kwamba kamati inajibu masuala ambayo Mjumbe ameyauliza wakati wa kuchangia na Waziri hakuweza kuyajibu. Hili la pili Mjumbe hakuchangia. Suala la *pound* 1,600 la riba kipindi hicho mimi nilikuwemo humo hata chooni kujisaidia sikwenda namsikiliza kila Mjumbe. Hili la pili sikulisikia kwa hivyo itakuwa ni mara yangu ya kwanza na kama anahitaji nimsaidie kujibu basi anipe muda nitakwenda kumtafutia majibu nitampa baadae.

Lakini la kwanza nataka nimjibu kama ifuatavyo. Tulipoanza na Benki ya Tanzania kwa makubaliano yetu wenyewe, mimi sikuwepo wakati huo bado nipo skuli mdogo, kwamba faida itakayopatikana iwe inarudishwa tena benki kama ni mtaji ili kukuza mtaji. Narudia, faida itakayopatikana iwe inarudishwa tena katika benki kama kuongeza mtaji. Sawa sawa na wewe Mhe. Mwenyekiti, unapokuwa na hisa unaweza ukawaandikia kwamba gawio langu lirudishwe ili iwe kama ni mtaji ndani ya hisa zangu, unaweza ukawaandikia kabisa kwenye hisa.

Kwa hivyo, muda wote huo tulikuwa tunarudisha mpaka mwaka 1992/1993 ndio tulipokaa tukaona sasa tuanze kutafuta gawio. Ndio wataalam walipokuja wakaja na hilo gawio la asilimia 4.5.

Ukitazama mtaji wa *BoT* Mhe. Mwenyekiti, sina kumbukumbu hapa lakini nilipokuwa Tanzania Bara nilikuwa ninautazama kila siku, mtaji wao umekua sana kwa sababu ya hiyo. Kukua kwa mtaji ndio na wewe unapata lile gawio linakuwa la kwako linaongezeka na kuwa kubwa. Kwa hivyo, katika miaka hiyo nataka nimwambie Mhe. Hija Hassan Hija kwamba tulizipeleka kule kama ni mtaji ili benki yetu iweze kukua.

Lakini hili la pili sijakataa kumjibu isipokuwa kwa sasa hivi sina majibu, nitamtafutia majibu baadae kwa sababu halikuja katika mchango wake.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, namshukuru kaka yangu lakini naomba nikubali kwamba nilikuja nalo kwa sababu nimelipata juu kwenye Maktaba ya Baraza nimeiona hiyo. Kwa hivyo, hili la pili nalikubali.

Lakini la mwanzo kama nimemfahamu ananambia faida iliyopatikana wakati huo Zanzibar tulikubali kwamba iwe ni sehemu ya ongezeko la mtaji. Nakubaliana kwamba wana utaratibu mzuri. Lakini naomba anielimishe je, sasa anakusudia kunambia kwamba tangu 1966 mpaka hii leo *share* yetu ya asilimia 11 na faida yetu ambayo imefanya mtaji mmesema tumepata milioni 800. Naomba anisaidie.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo nimsaidie ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine na Watanzania Wazanzibari wanaotuangalia.

Mhe. Mwenyekiti, hisa na faida vitu viwili tofauti. Hisa yako itabakia kama ni hisa yako mpaka mtakapovunja ule ubia, unatazamwa sasa mtaji wenu ni kiasi gani. Nataka nimpe mfano Mhe. Hija Hassan Hija. Kama tumeanza na benki shilingi 1,000 Zanzibar tukatia shilingi 300, ile ndio hisa yetu shilingi 300. Lakini leo kama benki yetu ina bilioni moja, hisa yetu sio shilingi 300, hisa yetu itakuwa shilingi milioni 300.

Lakini faida benki inafanya biashara, ikifanya biashara inaangalia nimepata faida kiasi gani baada ya kutoa *operational cost* zangu zote yaani gharama zangu za uendeshaji. Kile kinachopatikana sasa tunasema tumepata hiki, wewe nitakupa asilimia fulani na wewe asilimia fulani. Hizi asilimia za faida zinatakiwa zitoke kulingana na asilimia ya hisa nilizoweka. Lakini ndio kwa hapa kama nilivyosema asubuhi bado tunavutana na taarifa tulizonazo sisi tunasema hisa zetu ni asilimia 11 wao wanasema hatuna asilimia 11. Tunawauliza asilimia ngapi bado hawajasema asilimia ngapi.

Lakini hii asilimia ya 4.5 tunapata kulingana na wataalam ambao walioifanyia kazi wanasema anzeni na 4.5 baadae mnakwenda na hiyo *discussion*. Sasa hiyo ndio nataka nimfahamishe Mhe. Hija Hassan Hija.

Mhe. Mwenyekiti, pia ukitazama hata gawio kila biashara inapokuwa nzuri *dividend* yaani faida inakuwa nzuri na gawio letu nalo linakuwa zuri.

Kuna mwaka mmoja nadhani Mhe. Hija Hassan Hija naweza nikakupa kopi ninayo hapa, kuna mwaka mmoja hawakufanya faida *BOT,* kwa hivyo kama hawakufanya faida SMT hakupata faida, hakupata gawio na sisi hatukupata gawio. Nitakupa Mhe. Hija ninazo hapa taarifa zote nitakupatia.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, mimi namfahamu sana Mhe. Waziri na nakubaliana nae lakini hii kazi si nyepesi kiasi hicho. Sasa nimuombe tu na niwaombe wenzangu kwamba tumpe nafasi hoja hii pengine hadi mwakani ajipange atafute hizi kumbukumbu zote za hisa na ukweli wenyewe baadae atuletee turidhike sote Wazanzibari ambao wanataka kuona vipi tunafaidika kwa gawio hili. Sasa nadhani tumpe nafasi hiyo hoja yetu iendelee.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 1901 | Idara ya Utawala na Huduma | 9,760,504,000 |
| Kifungu 2101 | Idara ya Ukuzaji Uchumi | 111,100,000 |
| Kifungu 2201 | Idara ya Bajeti | |

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena nataka nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake na ufafanuzi. Lakini vile vile nataka nikiri kwamba kuna baadhi ya mambo kama ulivyoshauri Mhe. Mwenyekiti, tuwe makini sana serikali hasa inapotoka miongozo tunawafikia na wadau wengine. Kwa kweli suala langu lile la mwanzo kuna baadhi ya mahoteli mengi yaliathirika lakini hili limepita na namshukuru kwa maelekezo yake.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu iko hapa katika hii Idara ya Bajeti. Humu nilipoangalia katika vifungu vinavyoshughulikia idara hii kuna suala zima la *ZRB*.

Mhe. Mwenyekiti, tuliishauri sana serikali tokea tulipopitisha Bajeti ya Serikali kuhusu suala zima la serikali sasa hivi kuacha utaratibu wa ukusanyaji wa mapato kwa njia ya mkoba tutumie utaratibu wa *through bank*.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili Mhe. Waziri kutokana na muda hakuwahi kulitolea ufafanuzi. Lakini kabla ya kumpa nafasi nilikuwa nataka kidogo nitoe maoni yangu halafu katika majibu yake na yeye atanisaidia maelezo vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, fedha nyingi sana za serikali zinapotea na zaidi tukajaribu kuwalenga wakusanyaji wa mapato *ZRB* pamoja na *TRA*. Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana kuna wengine walielewa vibaya na hapa nilikuwa nataka kidogo nimsafishe Katibu Mkuu wa Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kwa sababu kuna vijineno neno vilikuwa vinazungumzwa kwamba labda mapato kuvuja tulimlenga Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha. Mhe. Mwenyekiti, Katibu Mkuu wetu ni mtu safi sana, ni mcha Mungu, Alhajj na ni mtu ambaye anaisaidia sana serikali mpaka kutufikisha hapa katika ukusanyaji wa mapato.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kama kuna watu walifahamu vibaya lengo nililowalenga wakusanyaji wetu Katibu Mkuu hashuki chini kwenda kukusanya pesa za leseni wala mambo mengine. Kwa hivyo, nilikuwa namsafisha ajisikie yupo huru kabisa na mimi sina tatizo nae ninamuamini na ninaendelea kumuamini na nitamuamini sana.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tatizo lililojitokeza sasa hivi fedha zinakusanywa hivi hivi tu watu wanakwenda wanapatana kama mtu anapatana fungu la muhogo. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi tunashukuru sana wenzetu Idara ya Uhamiaji kwa sababu wameanzisha utaratibu mzuri. Sasa hivi *passport* ni shilingi 50,000 tu. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi huendi na mkoba wako ukenda ukatia mkono mfukoni ukaletewa *passport* kidirishani, unakwenda zako benki unalipa. Idara ya Uhamiaji sasa hivi mapato yake mazuri tuangalie mpaka jengo walilojenga.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, serikali haijatoa tamko hapa lini tutaanza utaratibu wa mapato yetu kwenda kulipa benki. Baada ya maelezo ya Mhe. Waziri nikiridhika nitakaa kitako, sijaridhika nitampa na ushahidi wa pesa zinavyopotea.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi naungana na Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba Katibu Mkuu wangu ni mtu safi, ni mtu muadilifu, ni mchapa kazi, asiyechoka, anayependa watu na mimi Waziri wake ananisaidia sana. Naungana kabisa kabisa na Mhe. Hamza.

Lakini vile vile naungana na Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba umefika wakati hatuwezi tukafanya matumizi yoyote yale fedha ile ya serikali ikawa haiendi benki. Huo ni utaratibu potofu na ni utaratibu dhoofu. Jana nimeongea na watendaji wangu, *ZRB* na *TRA* walikuwepo, nimewapa muda wa mwezi wa Agosti mwisho sitaki kuona *transaction* yoyote ile inakweda pesa kwa pesa. Nimewaambia kinagaubwaga, sitomchukulia hatua mtoto mdogo, nitawachukulia hatua wao viongozi. Kuanzia ZRB na TRA na kwa hili niko *serious*. Kuna kamati imeundwa na Baraza la Mawaziri ya kusimamia mapato na kuhakikisha uvujaji tunaziba. Moja ni hili la kuhakikisha kwamba mapato yetu yote yanalipwa kupitia benki. Nataka nimwambie Mhe. Hamza tusaidiane, atakapoona mapato hayapitii benki aje aniambie na tutaona tutakavyowachukulia hatua.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri wetu kuwa msikivu na mchapakazi. Mhe. Mwenyekiti, nilipoeleza suala hili nilizungumzia, sio mapato kwa *ZRB* tu peke yake na *TRA*.

Mhe. Mwenyekiti, *TRA* mapato yetu yote yanapotea na wanapatana na mtu anaweza akamwambia katika 30 basi lipa 15, 5 nitakupa risiti. Masuala haya tunaona uchungu na ndio maana tukasema hii Mamlaka ya *TRA* sasa hivi kwani inashughuli gani, hii kazi kwa nini tusiwape *ZRB*. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tatizo tunaloliona mapato mengi yanapotea.

Mhe Mwenyekiti, nadhani kwa kuwa Mhe. Waziri alizungumza na watendaji wa *ZRB* basi tulilenga *ZRB*, *TRA* pamoja na taasisi nyengine. Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakupa mfano mmoja wenzetu Baraza la Manispaa mwaka 2000, mapato ya mwaka pale yalikuwa yanakusanywa milioni 400. Lakini Baraza la Manispaa liliunda tume ya madiwani wakafuatiliwa na wakafuatana na maafisa wale wanaokusanya kodi kule mguu kwa mguu. Mhe. Mwenyekiti, mapato yalizidi kwa asilimia 120. mapato yaliongezeka kutoka milioni 400 mpaka bilioni 1,200,000,000, hao ni manispaa peke yake kwa Mji wa Zanzibar. Ndio maana tukasema mheshimiwa tunawaonea huruma wafanyakazi wetu wastaafu wanalipwa pencheni ya Shs. 40,000. Lakini kuna vitoto vidogo vimeajiriwa kwa miaka miwili tu basi mtu anafungua nyumba kwa *remote*, yaani batara, sio jeuri batara, nyumba inafunguliwa kwa *remote* mlango. Mhe. Mwenyekiti, mapato yanapotea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini Mhe. Waziri akifuata ushauri wetu basi Zanzibar mapato yataongezeka. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa. Mimi huwa nakuonea tabu unapopanda kule kwenye kiti chako kisha ukazunguka nyuma kule ukavua koti, tukaja tukalifunika kitambaa hili rungu, yote hayo ni kwa kulinda utaratibu. Sasa utaratibu kwenye kamati sio kuchangia, ni kutafuta ufafanuzi tu. Nilikuwa naomba hili tu Mhe. Mwenyekiti, uliheshimu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mliponiona nilikuwa nataka nimzuwie, lakini nikakuona wewe, nilikuwa nataka nimwambie hilo, kwamba huo ni mchango na sisi hapa tunataka maelezo tu. Labda kwa *simplify* ile hoja yake ni kwamba serikali itasaidia nini kwa ajili ya *TRA* nao wakapitisha mapato yao benki, ndio hoja yake kubwa.

**Mhe Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze tena na mheshimiwa ndugu yangu Mhe. Hamza Hassan Juma. Mhe. Hamza ndio ndugu yangu mdogo zaidi kuliko hata Mhe. Hija Hassan Hija, anifahamu kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema jana nimekutana na *ZRB* na *TRA* nasisitiza tena *ZRB* na *TRA*. Nimeshamuomba Katibu Mkuu wangu yuko pale juu ananisikia nitafanya kikao na Makatibu Wakuu ambao wanakusanya fedha kwa kupitia

mawizara yao, wapo Makatibu Wakuu utawaona katika kasma za mapato tuliopitisha kuna fedha zinazokusanywa na mawizara. Nimemuomba Katibu Mkuu anitayarishie kikao hicho, ili na Makatibu Wakuu nao niwaambie, sasa hivi katika masuala ya mapato hatufanyi masihara.

Kwa nini hatufanyi masihara Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tumeongeza bilioni 50,000,000,000 bila ya kuongeza kodi. Kama hatujajikaza zitatushinda hizi kuzikusanya, ndio lengo langu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Kabla ya kuendelea Mhe. Waziri alipokuwa anatoa mtiririko wa sifa za Katibu Mkuu, nikasema huyu anafaa kwa kampeni, maana mtiririko wa sifa zile alizompa Katibu Mkuu anapita tu katika uchaguzi wowote. Ahsante sana tuendelee.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 2201 | Idara ya Bajeti | 19,666,570,000 |
| Kifungu 2202 | Chuo cha Uongozi wa Fedha | 1,058,000,000 |
| Kifungu 2203 | Bodi ya Mapato | |

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia nilimwambia Mhe. Waziri kuhusu majengo yanayojengwa ya *ZRB* na nikamwambia kwamba kwa kweli mnatumia gharama kubwa ya fedha kwa kujenga majumba makubwa, kama nchi za Ulaya na wakati sisi ni nchi maskini. Nikamtaka anipe hesabu ya majengo yanayojengwa na *ZRB*. Kwa bahati nzuri nashukuru kama amenitajia, lakini kuhusu suala hilo la kujenga majumba kwa gharama kubwa hakulizungumza, ingawa amenitajia hizi fedha.

Mhe. Waziri aliniambia kwamba sasa hivi wameshatumia shilingi bilioni 5 na *point*. Inategemea jengo hili mpaka kumaliza litatumia bilioni 7.2. Kwa hivyo, nilikuwa nataka maelezo zaidi, Mhe. Waziri aniambie kwamba hizi fedha zinatokana na serikali au tumekopeshwa na wahisani au zinatokana na sehemu gani, kwa sababu ni fedha nyingi sana ambazo zinatumika, wakati huku tuna matatizo zaidi watoto wetu wanakaa chini, hatuna vikalio skuli, madawa hatuna hospitali na wakati fedha zinazotumika ni nyingi kama hizi. Kwa hivyo nataka kujua.

**Mhe Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, nataka nimueleze tu kaka yangu, huyu ni kaka yangu Mhe. Subeit Khamis. Majengo mazuri asiyaogope sasa hivi ndio tunayokwenda nayo, tunataka tuibadilishe Zanzibar, tuwe na majengo yenye hadhi. Tunataka tuibadilishe Zanzibar tuwe tuna majengo yenye hadhi, asiogope gharama. Ukitaka jengo ambalo litaweza kufanya kazi na kukaa kwa miaka 20, 30 au 40 ni lazima utumie gharama kuweza kulijenga.

Vile vile aliuliza hizi fedha zinatoka wapi. Sisi Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo tumetiliana makubaliano na *ZRB*. *ZRB* ni wakala, tumetiliana makubaliano kwamba mtatukusanyia na kama ni wakala kuna *agency* pia ambaye unatakiwa kulipwa. Kwa hivyo, *ZRB* wenyewe katika zile fedha zao ndio wao wenyewe bakaa zao wanajua wanakuwa wanalipa ule ujenzi, *ZRB* wamechukua mkopo fedha zile kutoka kwa *ZSSF* na hivi sasa wanaendelea kumaliza kulipana kidogo kidogo kwa kila mwezi.

Kwa hivyo, taasisi kama hizi ambazo zinauwakala ni nzuri hasa ikaangalia uwezekano wa kujenga majengo mazuri.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Mhe. Mwenyekiti, nakubali anavyozungumza kwamba sasa hivi tunatakiwa tuwe na majengo mazuri na tusiyaogope. Lakini sasa tujiangalie sisi wenyewe na uwezo wetu tulionao. Kwa sababu sasa hivi wananchi wetu hawana dawa, watoto wetu skuli hawana vikalio, sasa atajenga jengo zuri huku vifaa muhimu huna. Ni sawa sawa na mtu kavaa kofia lakini huku chini hana buti. Sasa sisi tunajenga majengo mazuri ya ofisi lakini huko nyuma watoto wetu wanapata tabu.

Mhe. Mwenyekiti. Tuendelee.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 2203 | Bodi ya Mapato Ofisi Kuu | 5,434,000,000 |
| Kifungu 2204 | Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali | 860,000,000 |

Kifungu 2205 Mfuko wa Barabara

**Mahmoud Mohammed Mussa:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilimuomba Mhe. Waziri atuelezee juu ya suala la hoteli ya Mpapindi na hoteli ile ya *Venta Club*. Lakini alipokuwa akitoa majumuisho sikumsikia. Kwa hivyo, naomba ufafanuzi wa masuala hayo mawili.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mfuko wa Barabara huu.

**Mahmoud Mohammed Mussa:** Hapana. Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi. Bado haya tuendelee.

**Mhe. Mwenyekiti:** Nilikuwa namnong'oneza katibu hapa, kwamba anataka kuzungumzia barabara za ndani Kikwajuni pale.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 2205 | Mfuko wa Barabara | 6,432,000,000 |
| Kifungu 2206 | Mamlaka ya Uwekezaji | |

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Katika mchango wangu nilizungumzia suala zima la misamaha ya kodi na *ZIPA*. Nataka nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa majibu yake mazuri, fasaha na yenye kina katika suala hili. Namshukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kumuomba kitu kimoja tu. Wakati kipindi hiki yeye na uongozi wa wizara ya fedha unapoliangalia suala la kuleta marekebisho ya sheria ili kuziba yale aliyosema kwamba ni mianya, basi nilikuwa nataka kusema kwamba katika kipindi hiki aangalie sana suala la uvujaji wa mapato kwa kupitia maombi ya misamaha hii. Kwa sababu kama alivyotuambia mwenyewe kuna bilioni 50, ambazo anahitaji azitafute bila ya kuongeza kodi.

Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na tabia ya wenye mahoteli. Kwa mfano mtu keshajenga hoteli keshaomba punguzo kapewa apunguziwe, lakini bado anaendelea kuleta vitanda miaka na miaka bado anaomba apunguziwe. Anaendelea kuleta sahani na vikombe miaka baada ya miaka na hoteli imeshaji-*establish* na inatengeneza faida bado anaendelea kuomba punguzo. Nilikuwa namuomba Mhe. Waziri kwamba aliangalia suala hili kwa kipindi hiki, wakati anaangalia hayo marekebisho katika sheria zetu. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

**Mhe Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, nataka nikubaliane naye Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Nataka nimwambie kwamba yeye kama ni mwanasheria na wanasheria wengine ndani ya Baraza hili nitawaomba na wao wanipe maoni yao baada ya kuipitia ile sheria.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo katika suala la Mpapindi na *Venta Club*.

**Mhe. Mwenyekiti:** Hebu Mhe. Mjumbe, tupe ufafanuzi zaidi.

**Mahmoud Mohammed Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilimuomba Mhe. Waziri atuelezee juu ya suala la hoteli ya Mpapindi na hoteli ya *Venta Club*, ambazo zimekwama na shughuli zake, lakini bado wananchi wana madeni wanadai katika hoteli zile. Je, wizara yake imechukua hatua gani katika suala hilo, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niseme hivi Mhe. Makamo wa Pili ameunda kamati na mimi kama waziri ambaye nasimamia vitega uchumi, hajanikabidhi

ripoti nikaifanyia kazi. Kwanza tusubiri Mhe. Makamo wa Pili apatiwe hiyo ripoti, halafu baadae Mhe. Makamo wa Pili aipitie halafu atafute mawaziri wahusika, ikiwa na mimi ni mmoja wapo ili tuweze kuifanyia kazi. Namuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba avute subra tutamuarifu yatakayojiri.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 2206 | Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar | 300,000,000 |
| | **Jumla ya Fungu** | **47,020,008,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 45 MFUKO MKUU WA SERIKALI

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 9101 | Mfuko Mkuu wa Serikali | 47,819,800,000 |
| | **Jumla ya Fungu** | **47,819,800,000** |

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 19 OFISI YA RAIS FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 9401 | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 49,109,451,000 |
| Kifungu 0701 | Idara ya Muhasimu Mkuu wa Serikali | 20,000,000 |
| Kifungu 1001 | Idara ya Mipango ya Maendeleo na Watendakazi | 130,000,000 |
| Kifungu 1101 ya Sekta na | Idara ya Mipango ya Kitaifa Maendeleo Kupunguza Umaskini | 23,591,398,000 |
| Kifungu 1301 200,000,000 | Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma | |
| Kifungu 1901 | Idara ya Utawala na Huduma | 5,300,000,000 |
| Kifungu 2201 | Idara ya Bajeti | 1,866,480,000 |
| | **Jumla ya Fungu** | **80,217,329,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi, imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo bila mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liyakubali makadirio hayo.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji sasa wale wanaokubaliana na makadirio hayo wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

## HOJA ZA SERIKALI

## MSWADA WA SHERIA YA MAKISIO YA MWAKA 2011

**Mhe Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma kwa kutuwezesha kukaa, kuwasilisha, kujadili na kuidhinisha bajeti ya serikali pamoja na mpango wa maendeleo kwa mwaka 2011/2012.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi pamoja na wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuifanya kazi hiyo kwa umakini mkubwa na kutoa michango ambayo ni dhahiri itaimarisha utendaji wa serikali na kuleta tija zaidi kwa wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

Pili natoa shukrani zangu za dhati kwa Baraza lako tukufu chini ya usimamizi na uongozi wako mahiri kwa kupokea, kujadili na hatimaye kuidhinisha bajeti ya Wizara zote za serikali. Ninahakika michango yote iliyotolewa pamoja na ushauri katika maeneo mbali mbali ya kiutendaji itafanyiwa kazi kwa lengo la kuimarisha uchumi wetu, ustawi wa jamii na maendeleo kwa jumla.

Mhe. Spika, baada ya kueleza hayo sasa naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu mswada wa Sheria ya Matumizi kwa mwaka 2011/2012 kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ibara ya 106 inayomtaka waziri anayehusika na masuala ya fedha kuleta mswada huu kwa ajili ya kuidhinisha matumizi ya serikali.

Mhe. Spika, huu ni mswada wa sheria ya kuidhinisha makisio ya matumizi ya bilioni 613,076,460,000 kutoka mfuko mkuu wa hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia siku ya tarehe

30/06/2012, na kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha hizo, pamoja na mambo yanayohusiana na hayo kwenye Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, mswada huu wa makisio ya matumizi umedhamiria kutoa uwezo kwa serikali kutumia kutoka mfuko mkuu wa hazina jumla ya bilioni 613,076,460,000 kati ya fedha hizo bilioni 234,175,077,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida na bilioni 378,901,329,000 ni kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, kupitishwa kwa mswada huu kutaiwezesha pia serikali kukopa fedha kwa ajili ya matumizi sio zaidi ya tarehe 30/06/2012 kutoka ndani na nje ya Zanzibar. Kiasi cha fedha kilichoainishwa kwa ajili hiyo ni kulingana na masharti ya kifungu nambari 4.1 ya sheria hii.

Mhe. Spika, kifungu nambari 5.1 cha mswada huu kinatoa uwezo wa waziri mwenye dhamana ya mambo ya fedha kuruhusu maombi ya ziada kwa lengo la kukabili matumizi mengine ya dharura ambayo kama hayatoruhusiwa yatakuwa ni hasara kwa taifa kusubiri mpaka itakapoidhinisha tena na Baraza lako tukufu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa. Kabla hatujaendelea na majadiliano, niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe kwamba kazi mliofanya kuanzia tarehe 20, mwezi uliopita ya kujadili hotuba ya bajeti ya serikali na bajeti nyengine za wizara mbali mbali ndio tumemalizia hivi punde kwa wizara ya fedha.

Sasa anachoomba Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ni kuidhinishiwa fedha yote ile ya bajeti ya serikali ili serikali iweze kufanya kazi yake. Kama kuna hoja yoyote, nimwite Mhe. Ismaila Jussa Ladhu.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha wakati huu, tukiwa kama ulivyosema punde hivi tumekamilisha kazi nzito ya kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka huu wa 2011/2012, na sasa hivi tulikuwa tunajadili mswada huu wa sheria kwa ajili ya kuuidhinisha makisio haya ya mapato na matumizi kama ilivyoombwa na Mhe. Waziri hivi punde.

Mhe. Spika, kabla sijazungumza ninachotaka kuzungumza. Nataka nitumie fursa hii tu kusema kwamba nadhani Baraza letu limeweka historia katika kikao hiki. Imeweka historia kwa kuonesha kwamba mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa haujauwa ile dhana nzima ya Baraza hili kuwa ni chombo cha kuisimamia serikali. Katika hilo nataka niwashukuru na niwapongeze wajumbe wenzangu wote ambao kwa pamoja tumeifanya kazi hii.

Vile vile nataka niseme tu serikali pamoja na mawaziri watuelewe kwamba tumefanya vile kama mara nyingi tumekuwa tukiwakumbusha, sio kwa sababau yoyote ya nia mbaya, lakini ni kwa sababu ya kuhakikisha kwamba Baraza hili linafanyakazi yake ya kuiweka serikali jamvini na kuiwajibisha ili fedha za walipa kodi ziweze kutumika vile ambavyo imekusudiwa.

Mhe. Spika, hoja yangu niliyotaka kuigusia katika mswada huu ni moja tu. Huu mswada ni *appropriation bill*, na bila shaka tukiupitisha tutakuwa tumekamilisha ile kazi ya kuidhinisha matumizi haya ya serikali. Kulikuwa kuna nukta moja tu nilikuwa naomba Mhe. Waziri aitizame kwa makini na aisimamie. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tuna utaratibu mzuri wa kuwa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na anatayarisha ripoti ya kila mwaka ambayo inaletwa. Kwa hivyo, tumejadili mambo mengi na mengine tulikuwa tukiyadondoa dondoa.

Lakini kuna suala moja ambalo liko katika ripoti ya mwaka 2008/2009 tuliyowasilishiwa mwisho katika ukusara wa 28, naomba Mhe. Waziri alizingatie, ambapo sehemu hii inahusu wizara yake na wakati ule ilikuwa ikitiwa Wizara ya Fedha na Uchumi, nalo nimeandikwa kukosekana kwa *Appropriation Account* za wizara. Mhe. Spika, naomba ninukuu kidogo kwa sababu kama nilivyosema mchango wangu ni mfupi sana katika suala hili.

Ripoti ya *CAG* ya mwaka 2008/2009 ukurasa wa 28 unasema hivi:

> "Sheria ya Fedha ya Zanzibar Nam. 12 ya mwaka 2005 kifungu 24(2)(a) kinamtaka kila mdhamini wa fedha (*Accounting Officer)* wa Taasisi ya Serikali atayarishe orodha ya malipo aliyofanya kupitia vifungu vilivyopitishwa na Baraza na Wawakilishi.
>
> Ukaguzi uliofanyika kupitia Hesabu za Wizara ya Fedha na Uchumi umegundua wizara imeshindwa kuorodhesha na kuziwasilisha katika hesabu za mwisho wa mwaka kama sheria ilivyoagiza.
>
> Kutokana na hali hiyo, wakaguzi wameshindwa kujua uchambuzi halisi wa fedha kama zilivyotumika katika vifungu husika vya wizara.
>
> Aidha ukaguzi uliofanywa umegundua hakuka kumbukumbu zilizoingizwa katika hesabu za mwisho wa mwaka, kwa ajili

ya kuhalalisha na kulinganisha mapato yaliyoingizwa katika wizara kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali *Exchequer Issues and Notification*."

Mhe. Spika, naomba tu kwamba tunaingia katika mwaka mpya na bila ya shaka ripoti zitakuwa zinakuja kila wakati, kuwa mapungufu kama haya yaangaliwe kwa ujumla wake, ili fedha kama nilivyoelezwa kwenye ripoti hizi zinazoidhinishwa na Baraza lako kwa niaba ya walipa kodi wa nchi hii, basi ziweze kutumika kama zilivyokusudiwa.

Baada ya kutoa tanbihi hiyo Mhe. Spika, sina matatizo mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe naunga mkono mswada huu, pia namtakia kila la heri Mhe. Waziri katika kusimamia yale ambayo tumeyapitisha hapa. *(Makofi)*

Nakushukuru sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa machache katika mswada huu ambao Mhe. Waziri ameuwasilisha hivi karibuni.

Mhe. Spika, kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Vile vile niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wote kwa kazi ngumu tena nzito, ambapo wamekuja kutusomea bajeti zao, pamoja na kwamba waliona hali imebadilika, kama vile misukusuko midogo midogo, Mhe. Spika haya ni mambo ya kawaida katika mabunge yote duniani. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, kwa nini tulifanya hivi. Kwa kweli tumefanya hivi, ili yale ambayo Mhe. Rais wa Zanzibar anayoyataka yatekelezwa, kwa sababu tumezoea kufanyakazi kwa mazoea. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wale waliokuwa wanafikiria sisi labda tuna nia mbaya na serikali, basi michango yetu ndio itakayosema kama tulikuwa na nia mbaya na serikali au tulikuwa na nia nzuri kwa ajili ya kuisaidia serikali yetu. Kwa hivyo, naamini hata watendaji wetu serikalini hivi sasa watabadilika, pia naamini ule udokozi sasa utaondoka. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka tuwahakikishie sisi tukiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hatutokuwa tayari kumvumilia pamoja na kustahamilia mtu yeyote atakayedokoa mali ya serikali kuanzia hivi sasa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naamini Mhe. Waziri atakuja kutupa ushahidi kwamba haya makusanyo yaliyokuwa yanategemewa katika bajeti ya mwaka huu ya milioni 613, basi naamini Mhe. Waziri ukifika mwisho wa mwaka atatuambia kuwa mapato ya Zanzibar yameongezeka japo kwa asilimia 20 au 30. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba sana kama alivyozungumza ndugu yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwamba tunaomba sana serikali yetu ambayo kwa hapa mawaziri wetu ndio wanaotuwakilisha, basi yale matumizi ambayo tumeidhinisha tunaomba yale ndio wayatumie. Kwa kweli kuna jambo moja lilitokezea na nilizungumza kwamba tayari tulifanya malipo ya mwaka 2016, ambapo serikali itakayokuja ndio malipo yale ingeweza kuyafanya.

Lakini malipo yale tumeyaharakisha na kwa bahati mbaya sana Mhe. Waziri inaonesha hakufanya utafiti wa kutosha, malipo yale alisema labda tulikuwa tunaogopa riba. Mhe. Spika malipo yale hayakuwa na riba, kwa kuwa yameshafanywa, basi tunaomba kwa ile kazi ambayo tuliyoiagiza ifanywe. Hivyo, Mhe. Spika, naomba kazi ile ifanywe ili turidhike kwamba matumizi ya fedha za umma yanatumika vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya hayo machache mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura walionileta hapa tunaunga mkono Mswada huu wa Matumizi ya Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, pia nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, serikali ambayo inaongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein na humu ndani tunaye Kiongozi wetu wa Serikali Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa jinsi ambavyo walitusaidia kutuelimisha na kuwasaidia Wazanzibari kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, sisi kama Wawakilishi Mhe. Spika, tumeanzia hapa kama ni *Pilot Project* tukijaaliwa na mwaka itakuwa ni mradi kamili wa kuwasaidia Wazanzibari. Kwa hiyo, kila Mzanzibari, *backbencher* pamoja waziri asibweteke tufanyekazi kwa ajili ya kuwasaidia Wazanzibari. *(Makofi)*

Mhe. Spika, la pili nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha kwamba sisi Wajumbe wako katika ziara za kamati tulipita kwenye wizara tofauti na kila kamati imekuwa ikigundua, kwamba uingizwaji wa fedha kwenye wizara mbali mbali unakuwa hawendi vizuri, kama kwamba kujenga aaswira kuwa kuna wizara mama, wizara baba na wizara watoto.

Sasa namuomba Mhe. Waziri kwamba kila hali ya fedha ikipatikana vizuri basi kila wizara kwa vile ilivyoomba ipelekewe fedha kwa ajili ya mipango yake na utendaji kazi kwa kila wizara.

Vile vile nimuombe Mhe. Waziri kuwa utaratibu wa kuhaulisha vifungu, yaani *reallocation* hatuwezi kuuepuka. Lakini tukichukua hatua hiyo, basi lazima tuangalie vipaumbele ambavyo serikali yetu imeviangalia kulingana na vipaumbele vya serikali kwa bajeti hii.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, niseme tu kwamba kupitishwa kwa bajeti hii ni maandalizi ya bajeti ijayo, kwa hivyo tunategemea Wazanzibari kuwa itasimamia vizuri, ili mwaka haya yaliyotokezea tusiyaone tena. Kwa kweli Waswahili wa Vijijini wanasema ‘mtu akigangwa huambiwa maswibu uliyonayo huyaoni tena’ kwa hiyo tusifikie hatua hii.

Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wanachi wa Jimbo la Kiwani naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, naomba kwanza nikushukuru wewe kwa namna ambavyo ulilliongoza Baraza letu na unavyoendelea kuliongoza Baraza hili tukufu kwa umakini na umahiri mkubwa sana na kuweza kufikia hatua hii ambayo leo tumefikia. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Aidha nimshukuru Mhe. Waziri wa Fedha kwa namna ambavyo amewasilisha bajeti hii ya serikali. Kwa kweli niwashukuru pamoja na kuwapongeza sana watendaji wote wa wizara hii kwa umakini wao wa kuisaidia serikali na kufikia hatua hii nawashukuru sana. *(Makofi)*

Nataka nitumie fursa hii Mhe. Spika, kuwashukuru sana kwa kuanzia Mhe. Makamu wa Kwanza wa Pili wa Rais pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu kwa namna ambavyo wameendesha mijadala hii vizuri sana. Kwa kweli wameendesha mijadala kwa kutumia demokrasia yao, uwezo wa Kikatiba na kwetu tunaona ni mafunzo makubwa ambayo wametupa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka kuwahakikishia kwamba maelekezo na yale yote ambayo wametutaarifu, ili tujisahihishe kama serikali, basi tunachukua jukumu hilo la kurekebisha na kufanyakazi zetu kwa nidhamu na uadilifu mkubwa hasa kwenye matumizi ya serikali. *(Makofi)*

Jambo kubwa Mhe. Spika, ni mashirikiano na umoja wetu. Katika kufanyakazi kwenye Baraza hili tukufu Waheshimiwa Wajumbe na serikali hatuna budi kuwa na mashirikiano na umoja mkubwa sana, ili chombo chetu hiki chende vizuri kama kinavyokwenda. Kwa hivyo, mashirikiano yetu ndiyo yatatuwezesha kufikia hatua ile wananchi ambayo wanaikusudia serikali yao na Baraza lao hili tuyatekeleze. Hivyo, naamini kwa mwanzo huu mzuri basi tutaelekea katika mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda nilihakikishie baraza lako tukufu kwamba katika serikali tumejipanga kutekeleza wajibu wetu, ili kuhakikisha kuwa yale yote wananchi wanayoyahitaji kwa serikali yao yanatekelezwa. Vile vile zile ahadi zilizotolewa na serikali, basi zitatekelezwa kwa uadilifu pamoja na uaminifu mkubwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba mashirikiano ya wote na nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote pamoja na wananchi wote wa Zanzibar kwa namna walivyoshirikiana katika kusikiliza Baraza letu hili tukufu. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Spika, kwanza kabisa na mimi nataka nitoe shukurani zangu za dhati kwako kwa Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yao na hatimaye kuweza kupitisha *Appropriation Bill* kama nilivyoiwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba maoni ya waliochangia tukianzia na

1. Mhe. Jussa Ismail Ladhu,
2. Mhe. Hamza Hassan Juma,
3. Mhe. Hija Hassan Hija na
4. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. *(Makofi)*

Kwa kweli yote tumeyapokea na nataka niahidi kwamba tutayafanyiakazi hasa kwa kuzingatia kwamba, fedha hizi ni kodi za wananchi wetu na zina haja ya kurudishwa kwa wananchi wetu, ili faida yake waweze kuiona. *(Makofi)*
Mhe. Spika, nataka nimalizie kwa kusema kwamba niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi na tuendele kushirikiana, ili tuweze kufanikisha majukumu yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, naafiki. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mswada wa Sheria ya Makisio ya Mwaka 2011/2012**

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima, ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

**KAMATI YA BARAZA ZIMA**

**Mswada wa Sheria ya Makisio ya Mwaka 2011/2012**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 1 | - | Jina Fupi. |
| Kifungu 2 | - | Utoaji wa shilingi 613,076,406,000/= kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali. |
| Kifungu 3 | - | Makisio ya Fedha zinazokubalika. |
| Kifungu 4 | - | Uwezo wa Waziri Kukopa. |
| Kifungu 5 | - | Uwezo wa Waziri wa Maombi ya ziada. |
| Kifungu 6 | - | Marejesho ya Mkopo na Riba. |
| Kifungu 7 | - | Kukubaliwa kwa Mipango ya Maendeleo. |
| Kifungu 8 | | Kukubaliwa kwa Fedha zilizopitishwa kwa Matumizi ya Maendeleo. |

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali bila ya mabadiliko yoyote. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Spika, naafiki. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mswada wa Sheria ya Makisio ya Mwaka 2011/2012**

*(Kusomwa kwa Mara ya Pili)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Makisio ya mwaka 2011/2012 usomwe kwa mara ya pili.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu, katika kusomwa mara ya pili wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Katibu:** Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio ya Matumizi ya Shilingi Bilioni 613,076,406,000/= kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali kwa mwaka wa Fedha unaoishia siku ya tarehe 30 Juni, 2012 na Kuruhusu Utoaji wa Uhaulishaji Fedha hizo pamoja na Mambo yanayohusiana na hayo, sasa umepitishwa rasmi na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri tukapumzike. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, ni wazi kwamba tumefanyakazi kubwa na nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kazi kubwa mliyoifanya na kusaidia kiti kukamilisha kazi hiyo nafikiri ni vizuri.

Kwa kweli shughuli zetu zimebakia kidogo za miswada miwili ambayo hati zimewasilishwa pale asubuhi na wenyeviti walikuwa wako tayari. Lakini kutokana na kazi kubwa hiyo, basi nadhani tukubaliane kwamba shughuli hiyo tujipange vizuri tuimalize kwa kesho na kesho kutwa.

Sambamba na hilo tunampa nafasi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais akajitayarishe, kwa sababu na yeye ana kazi yake ya kumalizia shughuli zetu hizi. Kwa maana hiyo, tusitishe shughuli zetu hizi na kama kawaida na hoja hii

tuliipisha mapema kwamba kesho ni siku ya Jumamosi, kwa hiyo tunaendelea kwa mtiririko hadi saa 3:00 mchana, kama itakuwa tumemaliza shughuli mapema basi tunaweza kuamua vile tutakavyoona inafaa.

*(Saa 12:20 jioni Baraza liliahirishwa hadi tarehe 30/07/2011 saa 3:00 asubuhi)*